# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatano Julai 15, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580284

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Mapokezi makubwa yamsubiri Dk. Hussein Mwinyi Zanzibar

UKURASA 3


Fursa kuwabana wagombea si kampeni za kushangilia tu

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

Wasudan Kusini 'washerehekea' milio ya risasi, simanzi na vifo

Dokta Shein, mwenza aliyeaminiwa na Mkapa

UKURASA 11

# Ni mafuriko ubunge CCM

**IDADI** ya waliochukua fomu usipime, wasomi, madaktari, mawaziri, wasanii wajitosa... Wanahabari 10 wapanda 'ulingoni', Lema asema... *Endelea ukurasa 2, 3,4, 7 na 19*




## WADHAMINI WA LISSU WAWEKEWA PINGAMIZI


UKURASA 5

### SURA MPYA


Francis Nanai
**Kawe**


Mrisho Gambo
**Arusha Mjini**


Idda Mushi
**Moshi Vijijini**


Godfrey Simbeye
**Mbozi**


Fredrick Lowassa
**Monduli**


Zamarad Mketema
**Kinondoni**


Dk. James Jesse
**Segerea**


Dk. Charles Kimei
**Vunjo**


Askofu Gwajima
**Kawe**


Asha Baraka
**Kinondoni**


Emmanuel Maganga
**Mvomero**


Tarimba Abbas
**Kinondoni**


Tumaini Msowoya
**Iringa**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

Nipashe

Fursa kwa Wagombea! 2020

VOTE




Gazeti la Nipashe linatoa fursa kwa wagombea wote wa vyama vya siasa kunadi sera zao kupitia kurasa zetu kwa gharama nafuu.

Wasiliana nasi
The Guardian Limited
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz


**MICHEZO** SIMBA YATAJA WAKUSAJILIWA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla (kushoto), akirejesha fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea ubunge wa Jimbo la Nzega Vijijini kwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Nzega, Said Goha. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ni mafuriko ubunge CCM

**Na Waandishi Wetu**



Dk. Philip Mpango



Dk. Agelina Mabula



Innocent Bashungwa

NI Mafuriko. Ndicho kinachoonekana katika uchukuaji na urejeshaji fomu za kuomba ridhaa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini.

Waliojitokeza wengi ni waliowahi kuwa wabunge kwenye majimbo hayo kipindi kilichopita, waliokuwa wabunge hadi Julai, mwaka huu, mawaziri, naibu mawaziri, wanasheria, wasomi na wanataaluma mbalimbali.

Pia katika mchakato huo, wamo waandishi wa habari, wafanyabiashara, wakuu wa zamani wa taasisi nyeti, vijana na viongozi wa ngazi mbalimbali za serikali wakiwamo waliokuwa wakuu wa mikoa.

Licha ya mamia ya watu kupigana vikumbo kuwania ubunge majimboni kutoka katika makundi hayo, yako majimbo ambayo yametia fora kwa wingi wa watu likiwamo la Kibamba ambalo hadi jana lilikuwa na wanachama 88 waliochukua fomu. Jimbo hilo kabla ya kuanza mchakato, lilikuwa chini ya John Mnyika kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Katibu wa CCM wilaya ya Ubungo, Sylvester Yeredi, alisema wagombea wa kuomba ridhaa ya kuteuliwa kugombea katika majimbo ya Ubungo na Kibamba walianza kumiminika kuanzia saa 2:00 asubuhi.

Jimbo lililofuata kwa kuvunja rekodi ni Ubungo ambalo kuna wagombea 65. Mbunge wa Jimbo hilo katika kipindi kilichopita alikuwa SAEED Kubenea wa CHADEMA.

Katika wilaya ya Kinondoni yenye majimbo mawili ya Kawe na Kinondoni, Katibu wa CCM wa Wilaya hiyo, Sure Mwasanguti, alisema waliochukua fomu kwa jana walikuwa 80 kwa jimbo la Kawe na Kinondoni 31

Katibu wa CCM Wilaya ya Ilala, Iddi Mkoa, alitanabahisha kuwa katika jimbo la Segerea waliochukua fomu alikuwa 41, Ukonga 50 na Ilala tisa.

### MAWAZIRI WAJITOSA

Katika kinyang'anyiro cha ubunge, mawaziri sita walichukua fomu jana. Mawaziri hao ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (Buhigwe), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Joyce Ndalichako (Kasulu Mjini), Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (Vwawa), Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa (Karagwe), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Selemani Jafo ambaye anaomba ridhaa tena Kisarawe.

Wengine ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Palamagamba Kabudi (Kilosa), Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki aliyejitosa Jimbo la Same Magharibi.

Katika kundi hilo pia wamo naibu mawaziri Dk. Agelina Mabula wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Ilemela) na wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji Kondoa Mjini.

### SPIKA NA NAIBU WAKE

Aliyekuwa Spika wa Bunge la Tanzania katika bunge lililovunjwa, Job Ndugai, amejitokeza kuomba tena ridhaa katika Jimbo la Kongwa huku naibu wake, Dk. Tulia Ackson, akichukua fomu kuomba ridhaa ya kugombea Jimbo la Mbeya Mjini ambalo mbunge wake alikuwa Joseph Mbilinyi, maarufu kama Sugu.

Aidha, wabunge wa zamani ambao katika uchaguzi mkuu uliopita waliangushwa ama kwenye uchaguzi mkuu au wakati wa kura za maoni wamechukua fomu kujaribu kurudi tena.

Baadhi ya wabunge hao ni aliyewahi kuwa waziri katika serikali ya awamu ya tatu na ya nne, Prof. Juma Kapuya (Kaliua) na Abbas Mtemvu, Temeke.

Mbali na wabunge hao wa zamani, kinyang'anyiro cha ubunge pia kinawahusisha waliokuwa wakuu wa mikoa ambao hivi karibuni, ama walitenguliwa au kustaafu. Mmoja wa hao ni aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, aliyechukua fomu kugombea Arusha Mjini.

Wengine ni aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali (mstaafu) Emmanuel Maganga anayewania Mvomero na Aggrey Mwanry (Tabora) anayewania kurejea Siha baada ya kuangushwa katika uchaguzi mkuu wa 2015.

Pia, wamo viongozi wa dini kama Josephat Gwajima wa Kanisa ya Ufufuo na Uzima aliyejitosa Jimbo la Kawe na Mhadhiri wa Sheria wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. James Jesse, ambaye amechukua fomu Segerea.

Wengine waliojitokeza ni Frederick Lowassa ambaye ni mtoto wa Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mwananchi Communications Limited, Francis Nanai, ambaye ni miongoni mwa waliojitosa katika Jimbo la Kawe.

### WANAHABARI WAMO

Katika safu ya waliojitokeza kugombea ubunge, pia wamo wanahabari akiwamo mwandishi wa IPP Media Morogoro, Idda Mushi, anayewania Moshi Vijijini.

Waandishi wa habari wengine waliojitokeza ni Zamaradi Mketema (Kawe), Andrew Kuchonjoma (Songea Mjini), Cyprian Musiba (Mwibara), Tumaini Msowoya (Viti Maalum Iringa) na Hamisi Mkotya (Chemba).

# Wachambuzi wa siasa watoa sababu 'mafuriko'

**Na Gwamaka Alipipi**

WACHAMBUZI wa siasa nchini wamesema sababu ya kuwapo kwa mwamko mkubwa wa watu kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu za kuwania ubunge ni kupanuka kwa uwanja wa kisiasa nchini pamoja na kuhitaji kuteuliwa kushika nafasi za uongozi.

Wakizungumza na Nipashe wachambuzi hao pia wamesema sababu nyingine huenda ni njia mojawapo ya kupata maisha mazuri kirahisi, kukidhi mahitaji yao.

Tangu kufunguliwa kwa dirisha la kuchukua na kurejesha fomu za kuwania nafasi mbalimbali hususani ubunge kwa vyama vya siasa nchini, kumekuwa na 'utitiri' wa wagombea wanaojitokeza katika majimbo mbalimbali Tanzania Bara na Visiwani.

Hadi jana jioni, Nipashe ilishuhudia idadi kubwa ya wagombea wakijitokeza kuchukua fomu za kuteuliwa kuwania nafasi ya ubunge katika jimbo moja, huku mteule anayehitajika ni mmoja tu.

Akizungumzia hali hiyo, Dk. Bakari Mohammed kutoka Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema ubunge umeonekana kuwa ni 'dili' nyakati hizi.

"Wengine wamechukua fomu kwa ajili ya kuhudumia jamii, wengine wamechukua fomu kwa sababu wanataka ajira pamoja na kukidhi mahitaji yao," alisema Dk. Bakari.

Aliongeza kuwa: "Ni njia ya 'short cut' (fupi) ya kujikwamua kiuchumi, wengi wanadhani kwamba wakipata ubunge watakuwa wamejikwamua kimaisha. Lakini mwamko ni mkubwa kisiasa na tutarajie idadi kubwa zaidi."

Naye Dk. Richard Sambaiga, kutoka Idara ya Maendeleo ya Jamii, UDSM, alisema kilichobadilika mwaka 2015 na mwaka huu ni muktadha wa kufanya siasa pamoja na kupanuka kwa uwanja wa siasa.

Alisema idadi kubwa ya watia nia waliojitokeza majimboni wanatoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa sababu ya mabadiliko yaliyofanywa na chama hicho.

Dk. Sambaiga alisema miaka ya nyumba ndani ya CCM mgombea ambaye alikuwa hana pesa kushinda kura za maoni ilikuwa ni ngumu.

"Wanadhani uwanja wa kufanya siasa umepanuka, ile dhana kwamba ubunge ni kuwa na pesa imetoweka, Reform (mabadiliko) ndani ya chama ndiyo imewashawishi wanachama," alisema Dk. Sambaiga.

Pia Dk. Sambaiga alisema sababu nyingine ni wagombea kuhitaji nafasi za uteuzi siku zijazo.

"Wanahitaji kukumbukwa mbeleni kwenye uteuzi na hawa ni vijana, wameona kwamba ukipata fursa ya kuwania unaweza kukumbukwa."

Kwa upande wake wakili wa kujitegemea kutoka Mahakama Kuu ya Zanzibar, Othman Masoud, alisema sababu kubwa ni kuongezeka kwa kiwango cha elimu ya uraia.

Sababu nyingine aliitaja ni bunge lililopita lilishawishi watu wengi katika kuwania nafasi mbalimbali za uongozi, kutokana na hoja na mijadala iliyokuwa ikijadiliwa.

Alisema: "Hali ya kimaisha nayo imechochea, kote bara na visiwani, hali ya kimaisha ilibana sana hivyo wameamua kukimbilia kwenye ubunge ili kujikidhi kimaisha."

UCHAGUZI MKUU 2020

# Mapokezi makubwa yamsubiri Dk. Mwinyi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, anatarajiwa kuwasili leo mjini hapa na kupokewa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, asubuhi.

Baada ya kupokewa Dk. Mwinyi ataongozana na wafuasi wa CCM hadi Ofisi Kuu za CCM Kisiwandui na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Dk. Ali Mohamed Shein atamtambulisha rasmi mgombea huyo.

Atazuru kaburi la aliyekuwa Rais wa kwanza wa Zanzibar, marehemu Mzee Abeid Amani Karume na baadaye kufanyiwa tambiko na wazee maalum wa CCM ili kupata baraka zao.

Katibu wa Idara ya Itikadi na Uenezi wa CCM Zanzibar, Catherine Peter Nao, alisema maandalizi ya mapokezi yameshakamilika na wanachama kutoka mikoa mitatu ya Unguja watampokea mgombea huyo.

Alisema Dk. Mwinyi atazungumza na wazee wa CCM kwa kazi ya kupeperusha bendera katika uchaguzi mkuu wa Zanzibar pamoja na kuitangaza ilani ya uchaguzi ya chama hicho.

Pia, atazungumza na wanachama katika uwanja wa makao makuu ya CCM Kisiwandui kwa mara ya kwanza baada ya uteuzi wake wa kuwa mgombea wa urais wa Zanzibar.

"Hiyo ndiyo ratiba yetu fupi ya mapokezi ya mgombea wetu wa urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi... tumejipanga kumpatia mapokezi makubwa yenye shamra shamra mgombea wetu ambaye anakabiliwa na jukumu la kuhakikisha CCM inashika madaraka na kuongoza dola," alisema.




Katibu Mkuu wa Chama cha ADC, Doyo Hassan Doyo (kushoto), akimkabidhi fomu ya kuomba ridhaa ya kugombea urais kupitia ADC, Queen Sendiga, katika hafla iliyofanyika makao makuu ya chama hicho, Buguruni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Lema asema waletwe wote

**Na Mary Geofrey**

MWENYEKITI wa Kanda ya Kaskazini wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na aliyekuwa Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, amejitapa kushinda ubunge hata akishindanishwa na watia nia wote waliochukua fomu kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Lema amesema kama sheria ingeruhusu, angetaka wagombea wote wa CCM Arusha Mjini ashindane nao na kutamba kuwa angewashinda kwa kishindo.

Lema ambaye anatetea nafasi yake kwa awamu ya tatu mfululizo, aliyeleza hayo jana kupitia ukurasa wake wa Twitter.

"Nimesikia sikia majina ya wagombea ubunge Arusha Mjini kupitia CCM. Kama sheria ingeruhusu, wote 30 wangekuja kushindana nami na picha zao wote kutokea kwenye karatasi ya kura dhidi yangu, bado wangeimba wimbo walioimba 2010 na 2015. Twendeni mpaka mwanzo wa bahari, wepesi sana hawa," aliandika Lema kwenye ukurasa wake wa twitter.

Vilevile kwenye uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu, Lema aliwaambia wakazi wa Arusha hususani Jimbo la Arusha Mjini kwamba, watashinda.

"Tuna washinda tena. Msiogope," Lema aliwatia moyo wapigakura na wapenzi wa CHADEMA na wananchi wa jimbo lake.

CCM jana walifungua pazia kwa wanachama wake kuchukua fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea nafasi hiyo na miongoni mwa waliochukua fomu ni aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo.

Mchakato wa kuchukua na kurudisha fomu kwa wagombea wa nafasi za ubunge na udiwani kupitia CCM unatarajiwa kukamilika Julai 17, mwaka huu.



## NEC yahamishia Dodoma shughuli za uchaguzi mkuu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SHUGHULI za uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba mwaka huu, ikiwamo utoaji fomu za ugombea urais zitafanyika jijini Dodoma baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuhamia rasmi katika ofisi zake mpya zilizopo Njedengwa.

Tangu kuanzishwa kwa Tume hiyo ilikuwa ikifanya shughuli hizo katika ofisi tatu tofauti jijini Dar es Salaam ambazo ni jengo la Posta, ofisi ndogo ya Mtaa wa Garden na Bohari ambako hutumika kama ghala la kuhifadhia vifaa vya uchaguzi.

Akizungumza na kundi la kwanza la watumishi walioripoti katika ofisi hizo jijini hapa, Mkurugenzi wa Tume hiyo, Dk. Wilson Mahera, alisema hatua ya Tume kupata ofisi yake itaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake kwa kuokoa fedha na muda uliokuwa unatumika kutoka ofisi moja hadi nyingine.

Alisema shughuli za uchaguzi mkuu wa Oktoba ikiwa ni pamoja na utoaji wa fomu za uteuzi kwa wagombea wa urais katika uchaguzi huo sasa rasmi zitafanyika katika jengo hilo jipya lililopewa jina la Uchaguzi House.

Dk. Mahera aliwapongeza watumishi waliojitolea kutangulia Dodoma kwa ajili ya kuanza kazi katika ofisi hizo, huku akiwataka kujituma zaidi ili kazi zao ziakisi mwonekano wa ofisi hiyo.

T-MARC TANZANIA
Serving Communities, Improving Lives

**PUBLIC NOTICE**

**LOSS OF ORIGINAL MOTOR VEHICLE CARD**

We T-MARC Tanzania. do hereby announce the loss of Original motor vehicle registration card for Vehicle T 834 AXN which was reported to police station since 02/06/2020. For whoever finds it please kindly report it to the nearest police station.

**T-MARC TANZANIA**
**Plot # 215/217 Kuringa Drive, Bahari Rd, Tegeta Block D**
**P.O.Box 633266, Dar es Salaam, Tanzania**

# Mdee, Mkosamali, Mwakagenda wavuka mchakato CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

MCHAKATO wa kura za maoni wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa ajili ya ubunge katika majimbo mbalimbali, umeendelea kuwa moto, huku baadhi ya watiania wakongwe wakiibuka kidedea.

Wagombea waliopita ni pamoja na Halima Mdee (Kawe) (pichani), Sophia Mwakagenda (Rungwe) na Felix Mkosamali (Muhambwe).

Jimbo la Vunjo ni Grace Kiwelu, Tarime Mjini, Ester Matiko, Tarime Vijijini, John Heche, Ukonga ni Asia Msangi na Singida Mjini ni Rehema Mkoha.

Mdee pia alipitishwa katika kura hizo za maoni kwa ajili ya kugombea katika ubunge Viti Maalum (Kawe pamoja na Mwakagenda ambaye naye aliibuka mshindi kura za maoni Viti Maalum (Rungwe).

Wengine waliopitishwa ni Alinanuswe Mwalwange Jimbo la Kyela na Jumanne Masonda (Mufindi Kaskazini).

Wengine ni Emmanuel Lukumai (Bagamoyo), Boniface Mitole (Lulindi), Mansa Nyuchi (Nanyumbu), Magharibi Gervas Mgonja (Same Magharibi)) na Rhoda Kunuhela (Mpanda Mjini).



Kwa upande wa viti maalum waliopita ni Severine Martin (Bagamoyo) na Tamali Mwambalaswa (Kyela).

Mwimbaji nyimbo za injili akwama

Katika Jimbo la Kyela, mwimbaji wa nyimbo za Injili, Martha Mwaipaja, aligombea na kushindwa kwa kupata nafasi ya tatu kati ya watu watatu waliokuwa wakiwania nafasi hizo.

Taarifa ya matokeo hayo kwa baadhi ya majimbo ilitolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema.

# Mamia wapigana vikumbo majimboni

**Na Waandishi Wetu**

MAMIA ya wanachama wa Chama cha Mapinduzi, jana walianza kupigana vikumbo majimboni kwa ajili ya kuchukua fomu za kuwania kuteuliwa kugombea ubunge katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Katika Jimbo la Arusha Mjini, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amejitosa sambamba na mwanahabari Swalehe Kiluvia, Alpha Laizer, Steven Lyamuya, Mustafa Panju, Ambroce Malai, Humphrey Soka, Hillary Mollel, Anna Mwambapa,Thomas Munisi, Loota Laizer, Ezra Mollel na Pamella Mollel.

Wengine Phillemon Monaban, Lomollo Ole Mollel, Juma Makwara, Noel Ole Valoya, Baraka Lukumay, Sambweri Lotta, Anald Manane, Mstahiki Meya aliyejiuzulu, Kalisti Lazaro

Katika jimbo la Longido walioomba ridhaa ni Dk. Steven Lemono, Justine Logotu, Wakili Ntasikoi Ole Senteu, Francis Ole Ikayo, Pamphil Olduka, Lairumbe Laizer, Nicholaus Senteu, Martha Ntoipo, aliyekuwa Mbunge wa jimbo hilo mwaka 2015, Onesmo Ole Nangole na Sabore Ole Moloimet,

Kwa jimbo la Karatu aliyekuwa amejitokeza hadi jana jioni ni Mkurugenzi wa Chama cha Wajane Tanzania (TAWIA), Rose Sarwatt,

**DAR ES SALAAM**

Walioomba jimbo la Kawe ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mwananchi Communications Limited, Francis Nanai, Kiongozi wa Kanisa ya Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, Magori Alphonce, mwanafunzi wa udaktari mwenye umri wa miaka 24, Rosemary Shungi,

Jimbo la Kinondoni ni Tarimba Abbas, Asha Baraka, Zamaradi Mketema, Nawab Mulla, Rajabu Said na Kelvin Berege.

Jimbo la Kibamba waliochukua fomu ni 88, Jimbo la Ubungo ni 65, Segerea 41 na Ukonga 50 huku Temeke yenye majimbo ya Mbagala na Kigamboni, wanachama 79 wamejitokeza.

**DODOMA**

Waliochukua Dodoma Mjini ni Adam Msendo, Amos Msanjila, Eliud Mazengo, Robert Mtyani, Josephat Ngomeni, Victor Mkama, Mohamed Mgoli, Vannesa Marika, Nollasco Mlay, Adam Amos na Michael Malecela.

Wengine ni Robert Mwinje, Gregory Kuzenza, Tadei Mwanga, Jackson Mashine, Masuala Shedrack, Said Mawazo, Julius Liwenga, Rashid Khamis, Mwajuma Mohammed, Dennis Guluse na Frank Supa.

Jimbo la Kondoa Mjini ni Edwin Sannda, Ali Makoa, Fausta Isuya, Dk. Ramadhani Mchana, Omary Kimbisa, Naima Chondo, Abdalah Isele, Hamisi Bea, Seleman Abdulrahman, Juma Kangaa, Dk. Jacob Lubuva, Ismail Saidi, Dk. Mzamiru Mwinyilago, Hassan Misanya, Selemani Sungi, Saidi Kidangi, Halfa Lubuva na Theresia Kibao.

Kondoa Mjini ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, Habiba Bowu na Issa Orry wakati jimbo la Chemba ni Emmanuel Taghali, Amasha Ninga, Sona Muslim, Tangerine Nkusa, Dk. John Lassa, Mwalimu Dickson Issujah, Juvens Class, Dk. Rogath Mhindi, Francis Julius, Hamis Mkotya, Dk. Adelini Mtunya na Juma Suru.

Jimbo la Chilonwa ni Deogratius Ndejembi, Philip Chiwanga, Mary Lubeleje, Rehema Kayombo, Nyemo Chiwaligo, Joel Mwaka, Amanita Msage, Elisha Mwalimu, Assad Bandi, Jerome Balisidya, Gabnel Masinge, Andrea Nyemba, Daniel Chisaluni, Bill Chidabwa, Theoderist Makuzini, John Chigongo, Emmanuel Chidong'oyi na Nathan Chibehe.

Jimbo la Mtera waliochukua ni Amos Mmemo, Happiness Mugongo, Dk. Michael Msendekwa, Amos Hoya, Mwanga Chibago, Silvesta Ndalu, Richard Masimba, John Makota, Jacob Mkonge, Haruna Mlagaza, Baraka Mkunda na Livingstone Lusinde.

Aidha, aliyekuwa Spika wa Bunge la 11, Job Ndugai, amechukua fomu Jimbo la Bahi na waliochukua fomu ni wanachama 17, huku Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, aliyechukua fomu jimbo la Kibakwe.

**KILIMANJARO**

Jimbo la Siha ni Aggrey Mwanri, Tumsifu Kweka, Meijo Laizer, Dk. Godwin Maimu, Wilhem Nkini na Evance Mushi, Leoanrd Massawe, Ephata Kaale, Mhandisi Betson Maimu, Eunice Mmari,David Bakari, Goodluck Nnko, Gadiel Massawe, Godson Ngomuo na Godbless Mwandry.

**SINGIDA**

Aliyekuwa mbunge wa jimbo la Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, amechukua fomu kuomba ridhaa kugombea ubunge huku Mtangazaji Harris Kapiga akichukua kuwania Iramba Mashariki.

**MBEYA NA SONGWE**

Aliyekuwa Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, alichukua fomu kuomba ridhaa ya kuwania ubunge Mbeya Mjini huku Mkurugenzi Mtwendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Godfrey Simbeye, akijitokeza kugombea Mbozi. David Silinde, aliyekuwa mbunge wa Momba kupitia CHADEMA, anawania kupitia CCM.

# Mwinyi aahidi 'ruksa' Zanzibar

**Na Mary Geofrey**

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussen Mwinyi, amesema akichaguliwa kushika nafasi hiyo, ataienzi kwa vitendo kaulimbiu ya 'ruksa' ya Rais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi.

Kaulimbiu hiyo ilimfanya Rais Mwinyi aitwe 'Mzee wa Ruksa' na Dk. Mwinyi ameielezea kuwa ilimpa baba yake umaarufu mkubwa kutokana na utashi wake wa kuruhusu biashara za aina mbalimbali kufanyika nchini, ili kufungua milango ya uchumi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo katika mahojiano yake na Kituo cha Televisheni cha Azam jana, akiahidi kuwa hilo ni moja mambo atakayoyafanya Zanzibar.

Katika mahojiano hayo ya kwanza kwake tangu ateuliwe na Mkutano Mkuu wa CCM kuwania nafasi hiyo Julai 11 mwaka huu, Dk. Mwinyi alisema Rais Mwinyi aliruhusu biashara zote zifanyike, ili kufungua uchumi wa soko na kuleta maendeleo ya Bara na Zanzibar.

"Ni jambo ambalo nitalienzi kama Rais wa Zanzibar kutoka kwa Mzee Mwinyi na nitalitekeleza katika utendaji kazi wangu," alisema.

Vilevile, alisema hakuwa kufanya kazi na Mzee Mwinyi kwa karibu kama Marais wastaafu Benjamin Mkapa, Dk. Jakaya Kikwete na Rais wa sasa, Dk. John Magufuli, ambao ana mengi ya kujifunza kutoka kwao.

Alisema atayaenzi mema yote waliyotenda wakati wakiwa madarakani na kuendelea kusisitiza kuwa, atafanya kazi kwa kurudisha bidii, nidhamu na kuondoa rushwa kama ambavyo anafanya Rais Magufuli.

"Sikutarajia tutafikia idadi ile (wakati wa mchakato uteuzi), lakini ndiyo siasa sababu utaratibu mzuri wa demokrasia, chama chetu tungeweza kuwa wengi hata uchaguzi wa mwaka 2015 walikuwa 42 (watia nia urais wa Tanzania), ni utaratibu wa kila anayetaka kugombea anagombea. Mimi niliwahi kuchukua fomu sababu nilikuwa na nia,"alisema.

Kuhusu aliyemshawishi kuchukua fomu, Dk. Mwinyi alisema: "Siwezi kusema kuna mtu maalum, mimi mwenyewe baada ya miaka 20 kuwa mbunge na 20 waziri, niliona nimeshakuwa mzoefu na wakati umefika kugombea urais.

Alisema aliwahi kuwa mbunge kutoka Zanzibar kwa miaka 15, hivyo alijiona miongoni mwa wanaofahamika kama wagombea wengine na anayestahili kuwania nafasi hiyo tofauti na wengi wanavyodhani kuwa yeye ni wa Tanzania Bara.

"Ninamshukuru Rais Magufuli kwa maamuzi yake mazuri ya wazi na mazuri, ingawa tulishangaa kwa sababu hatukuwa tumezoea upigaji kura wa wazi, tuliondoka pale kwa amani na haki kila mtu akitambua matokeo yake ni halali," alisema.

Dk. Mwinyi pia alitolea ufafanuzi madai ya kwamba wajumbe kutoka Zanzibar hawakumpigia kura, akisema siyo ya kweli, akisema kuwa anaamini bila kura kutoka upande huo wa muungano, asingefikisha idadi ya kura alizopta.

"Wajumbe wa Zanzibar ni 68, wenzangu (washindani wake wawili) walipata kura 35," alifafanua.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kulia), akionyesha tuzo aliyokabidhiwa na Waziri wa Viwanda na Biashara wa Zanzibar, Balozi Amina Ally (wa pili kushoto) kwa ajili ya kutambua mchango wa benki hiyo kama mdhamini mkuu wa Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa yaliyofungwa jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WCF yatwaa tuzo Sabasaba

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), umetwaa tuzo ya mshindi wa kwanza ya Mwonyeshaji Bora Kundi la Taasisi za Bima na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwenye Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa jijini Dar es Salaam, maarufu Sabasaba.

Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Masha Mshomba, alipokea tuzo hiyo kutoka kwa Waziri wa Viwanda na Biashara wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Balozi Amina Salum Ali, wakati wa kilele cha maonyesho hayo kwenye Viwanja vya Julius Nyerere jana.

"Kusema kweli siku ya leo (jana) tunayo furaha sana. Mimi mwenyewe na wafanyakazi wenzangu wote kwa mara ya kwanza tumeshika nafasi ya kwanza katika sekta ya bima na mifuko ya hifadhi ya jamii.

"Hii inadhihirisha kwamba penye nia pana njia. Mwaka jana, tulikuwa washindi wa pili, tukaweka azma kwamba wa walau siku moja tuwe washindi wa kwanza na leo imefika, tunashukuru sana.

"Ushindi huu unaendana na dira yetu ya mfuko, tumejiwekea malengo ya kuwa taasisi ya kuigwa siyo tu hapa Tanzania, bali Afrika hususan katika taasisi za hifadhi ya jamii na haswa katika mifuko ya fidia na tunapokuwa wa kwanza katika maonyesho haya makubwa nchini, hiyo inaonyesha kwamba tuko katika njia sahihi na lengo letu ni kuendelea kushika nafasi kama hizi katika maonyesho na shughuli mbalimbali tunazoshiriki.

"Huduma zetu ni bora, tumeboresha sana huduma zetu na kwa sasa zinapatikana kupitia mtandao na waliofika katika banda hili wameelezea jinsi walivyovutiwa na huduma zetu zote zinazopatikana kupitia mtandao na ule usumbufu kwa wateja haupo kabisa kwa sababu mafao yanalipwa kupitia mtandao."

Mkurugenzi huyo alisema taarifa za kutokea ajali au kuumia kazini pia zinawasilishwa kupitia mtandao sambamba na usajili wa waajiri na wanachama wenyewe.

"Kila kitu kwa sasa tunafanya kupitia mtandao. Usajili wa waajiri ni kupitia mtandao, ukusanyaji wa michango ni kupitia mtandaoni. Kwa hiyo, kila kitu tunafanya kwa kutumia mtandao na hilo kwa kweli limewezesha kuboreshwa kwa shughuli zetu na nia yetu ya kuwa kileleni," alitamba.

# Wadhamini wa Lissu wawekewa pingamizi

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri umewasilisha pingamizi la awali mahakamani kupinga maombi yaliyowasilishwa na wadhamini Ibrahim Ahmed na Robart Katula wa mbunge wa zamani wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, ukidai kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza na kutaka maombi hayo yatupwe.

Katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wadhamini hao wamefungua maombi wakiitaka itoe hati ya kumkamata Lissu kwa kuwa wao wameshindwa kumpata.

Kesi hiyo imetajwa jana katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upande wa Jamhuri unaomba maombi hayo kutupiliwa mbali kwa sababu mahakama hiyo haiwezi kushughulikia jambo hilo.

Alidai kuwa kupitia hati ya kiapo kinzani mahakama hiyo haiwezi kusikiliza na kutolea uamuzi wa maombi hayo ya walalamikaji na yatupwe.

Walalamikaji wanaomba mahakama itoe hati ya kumkamata Lissu kwa kuwa wameshindwa kumpata na kumfikisha mahakamani hapo.

Hati ya pingamizi la awali, iliwasilishwa mahakamani na Wankyo kwa sababu ndiye aliyepewa mamlaka ya kuendesha kesi ya msingi na maombi hayo.

Maombi hayo, yalipangwa jana mbele Hakimu Simba kwa ajili ya kusikiliza.

Hata hivyo, Wankyo aliomba mahakama itoe siku 14 ili aweze kujibu maombi hayo kwa njia ya maandishi.

Wankyo alidai kuwa anaomba siku hizo ili aweze kupitia jalada la kesi ya msingi na pia kupitia kesi mbalimbali ambazo zilishatolewa uamuzi.

Hata hivyo, mmoja wa wadhamini hao (Katula), aliomba muda wa kujibu pingamizi hilo na hakimu alisema kisheria pingamizi la awali ndiyo linatakiwa kuanza kusikilizwa.

Hakimu Simba aliwauliza wadhamini hao kama wanapingamizi na suala la upande wa Jamhuri kuwasilisha majibu yao kwa njia ya maandishi na waleta maombi walidai kuwa hawana pingamizi.



Alisema upande wa Jamhuri unatakiwa kuwasilisha majibu hao Julai 28, 2020, waleta maombi wanatakiwa kujibu hoja hizo Agosti 11, 2020, kama kuna majibu ya ziada yatawasilishwa Agosti 18, 2020 na kesi itatajwa Agosti 19, mwaka huu na kupangwa tarehe ya uamuzi.

Wankyo alidai katika majibu yake hati ya kiapo kilichowasilishwa mahakamani na waleta maombi hao kwa Lissu aliruka dhamana toka tarehe ambayo alipona na kutoka hospitali.

Alidai kuwa wadhamini hao walikuwa na taarifa za kutosha mahali alipo kwa sababu ilitangazwa na alieleza hivyo hivyo mahakamani, kwamba wadhamini wa mshtakiwa namba mbili (Lissu) wana wajibu wa kuhakikisha kwamba anafika mahakamani kwa mujibu wa amri ya mahakama iliyotolewa Januari 20, mwaka huu na hakimu Simba.

Kesi ya msingi imeahirishwa hadi Agosti 18, mwaka huu.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Wahariri Simon Mkina, Jabir Idrisa na Mchapishaji wa Kampuni ya Jamana, Ismail Mehbooh.

Katika kesi ya msingi kwa pamoja washtakiwa hao, wanakabiliwa na mashtaka matano ikiwamo kuandika habari za uchochezi kinyume na Sheria ya Magazeti ya mwaka 2002.

**BANI INVESTMENT LIMITED**
**DEBT COLLECTORS/ AUCTIONEERS**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KWA WADAIWA WA NBC BANK MAKAO MAKUU DAR ES SALAAM**

Kwa idhini tuliyopewa na **BENKI YA NBC MAKAO MAKUU** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara mali zilizoorodheshwa hapo chini ambazo ziliwekwa kama dhamana ya mkopo. Mnada utafanyika mahali zilipo mali hizi, siku na saa kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

| JINA LA AKAUNTI | MMILIKI | MALI ZILIZOWEKWA DHAMANA | MAHALI | TAREHE | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| Kinson Enterprises C | EXAUD KIMSON TEMU | Nyumba yenye plot no 267 block "Q4" | Kibamba-Dar es salaam | 29.7.2020 | 4:00 asubuhi |
| Nashoni M.Nyamhanga | JAMES POLISI | Nyumba yenye CT NO.114412, PLOT NO.1047 BLOCK E · | Tegeta-Dar es salaam | 4.8.2020 | 4:00 asubuhi |
| METRWA ENTERPRISES | SILVANUS MEDARD SOKO | Nyumba yenye CT NO.85569, L.O. NO.407200, PLOT NO.814 BLOCK 'E' | Goba-Dar es salaam | 4.8.2020 | 6:00 mchana |
| Wilson J Sanga | TUHANGILE JOTHAM SANGA | Nyumba yenye CT NO. 9726, L.O.NO. 107434,PLOT NO. 44,BLOCK 'G' | Makambako | 29.7.2020 | 4:00 asubuhi |
| Anjela W. Mwalongo | PAULO JOTHAM SANGA | Nyumba yenye CT NO. 13686 - MBYLR L.O NO. 364443 PLOT NO. 119 BLOCK 'P', | Makambako | 1.8.2020 | 4:00 asubuhi |
| Felix Simon Mtivike | FELIX MTIVIKE | Nyumba yenye CT NO. 13686 - MBYLR L.O NO. 364443 PLOT NO. 119 BLOCK 'P' | Makambako | 1.8.2020 | 6:00 mchana |
| Solomon G Kalambile | Solomon G Kalambile | Nyumba yenye CT.NO.14650-MBYLR, PLOT.NO.389, BLOCK 'O' | Njombe | 30.7.2020 | 4:00 asubuhi |
| Gaudete Gen Supplies | TUHANGILE JOTHAM SANGA | Nyumba yenye C.T NO. 9020 Plot No. 515 Block D | Njombe | 30.7.2020 | 4;00 asubuhi |
| Yahaya B Ndondole | BENJAMIN NDONDOLE | Nyumba yenye CT NO. 9816 MBYLR L.O NO. 185560 PLOT NO. 126 BLOCK 'G' | Njombe | 1.8.2020 | 4;00 asubuhi |
| Jossia Robert Sanga | Jossia Robert Sanga | Nyumba yenye CT.NO.11542-MBYLR PLOT NO. 45 BLOCK 'G' | Njombe | 1.8.2020 | 6:00 mchana |
| Michael E. Mtweve | LAURENCE SHAURITANGA MTWEVE | Nyumba yenye CT. NO. 1992-MBYLR LO NO. 95647 PLOT NO. 2,BLOCK E LUDEWA | Ludewa-Iringa | 4.8.2020 | 4:00 asubuhi |
| Ally Isidori Ilomo | ALLY ISIDORI ILOMO | Nyumba yenye CT NO.15706-MBYLR, L.O.NO. 189521, PLOT NO.24 | Nkuyu-Kyela | 4.8.2020 | 4:00 asubuhi |
| Julius J Mnungah | Julius J Mnungah | Nyumba yenye C.T. NO. 10672-MBYRL PLOT NO. 260 BLOCK'C' | Uyole-Mbeya | 7.8.2020 | 4:00 asubuhi |
| Francis M Mutombu | FRANCIS MAWIT MUTOMBU | Nyumba yenye CT NO.11841-MBYLR, L.O. NO.294806, PLOT NO.11 | Mbozi-Mbeya | 11.8.2020 | 4;00 asubuhi |
| Robert Charles | FRANCIS MAWIT MUTOMBU | Nyumba yenye CT NO.11949 PLOT NO 30 BLOCK C | Ubaruku-Mbeya | 13.8.2020 | 4;00 asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mali zitauzwa "kama zilivyo " as is where is basis"
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wowote isipokuwa usiku.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Ofisi ya:
Kwa maelezo zaidi wasiliana Na ofisi ya BANI INVESTMENT LTD
Nkurmah Street, Lida Building, Ghorofa ya 3, Chumba No. 0313 S.L.P 71340
Dar es Salaam au kwa simu na. 0713 224 578, 0713 295747, 0653 640 999,0713 295 747

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaosaka uongozi wawe watumishi wa wananchi

MCHAKATO wa kusaka uongozi wa nchi yetu ngazi ya udiwani, ubunge na urais kwa kupitia uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba, sasa ni rasmi.

Ni rasmi kwa sababu baadhi ya vyama vimeanza kupata wagombea, huku vingine vikiendelea na mchakato wa kuwashindanisha kupitia kura za maoni.

Karibu kila chama hivi sasa kiko katika pilikapilika za kuhakikisha kinakamilisha mchakato wa kupata wagombea kabla ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutangaza ratiba rasmi ya uchaguzi kuhusu. Mchakato wa NEC unahusisha uchukuaji fomu, urejeshaji, mapingamizi, uteuzi, kampeni na upigaji kura.

Jambo moja kubwa tofauti na miaka iliyopita ya uchaguzi mkuu, safari hii wamejitokeza watiania wengi katika vyama vya siasa ambao wanaomba kuteuliwa kupeperusha bendera za vyama vyao.

Idadi kubwa ilishuhudiwa katika Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) katika baadhi ya majimbo, lakini pia jana ikiwa siku ya kwanza kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuanza uchukuaji wa fomu za uteuzi hali hiyo ilijirudia.

Kuna majimbo ambayo waliochukua fomu wameanzia zaidi ya 40 hadi kufikia 40 huku mchakato huo ukiendelea hadi Julai 17, mwaka huu.

Ingawa uchukuaji fomu haujaanza katika baadhi ya vyama, lakini kujitokeza kwa wanachama wengi kutaka ubunge ni ishara kwamba demokrasia imechipukia ndani ya vyama vya siasa.

Inawezekana kuwa kuna sababu zingine zilizohamasisha wengi kuchangamkia kugombea, ikiwamo kuamini kuwa haki itachukua nafasi kutokana na dhamira ya dhati ya serikali ya kudhibiti vitendo vya rushwa kwa kuipa 'meno' Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwakamata na kuwachukulia hatua wale watakaobainika kujihusisha na rushwa.

Tunaona hivyo kwa kuwa huko nyuma kulikuwa na ugumu kwa mtu kwenda kugombea ubunge au udiwani bila kuwa na fedha nyingi kwa ajili ya kutafuta kuungwa mkono na wajumbe wanaopitisha wagombea katika vikao vya vyama na vile vile kwa wapigakura wakati wa mchakato wa uchaguzi.

Ni jambo la kufurahisha kuona wanachama wa vyama vya siasa kuchangamkia kugombea nafasi za uongozi kwa ajili ya kuwatetea na kuwaletea maendeleo wananchi. Hali hiyo inaonyesha jinsi gani kila mmoja alivyo na haki ya kikatiba ya kuchagua na kuchaguliwa.

Hata hivyo, ushauri wetu walioshajitokeza na watakaojitokeza baadaye kuomba nafasi za kuteuliwa kuwania urais, ubunge na udiwani ni kuwa na nia na dhamira ya dhati ya kuwatumikia wananchi naTanzania kwa ujumla.

Hatutarajii kuona mtu anasukumwa na maslahi binafsi kwenda kugombea nafasi anayoombea uteuzi hususan kupata fedha, maana kuna dhana iliyojengeka nchini kuwa njia rahisi ya kupata utajiri ni kuwa mbunge.

Tunawakumbusha waliojitokeza kwamba ubunge ni utumishi wa umma, hivyo nafasi hiyo inawahitaji watu wanaokerwa na matatizo ya wananchi, ambao watakwenda kuyazungumza kwenye vikao vya uamuzi vya Bunge na Mabaraza ya madiwani ili yapatiwe ufumbuzi.

Yako pia matatizo yanayoikabili Tanzania kama Taifa, hivyo yanawahitaji watu wenye nia ya dhati ya na uwezo wa kuishauri serikali kupitia Bunge kwa lengo la kuyatafutia ufumbuzi.


Wakati huu hauwahitaji watu wasio na sifa za utumishi kwenda bungeni kwa sababu tu wamewapa rushwa wananchi wakawachagua

Tunatoa rai kwa vyama vya siasa kuwa makini katika michakato yao ya uteuzi wa wagombea wao ikiwamo kutenda haki, kuteua wagombea wenye sifa zilizoainishwa pamoja na uadilifu, uaminifu, weledi na ujasiri.

Tunatarajia kuwa la jinsia litapewa kipaumbele; kwa maana kundi la wanawake pamoja na kutoa nafasi wanazostahili watu wa makundi mengine maalum ya vijana na watu wenye ulemavu.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge

# Kulikoni wimbi hili ubunge, udiwani CCM?



Na Mary Geofrey

UCHAGUZI mkuu wa mwaka huu unashuhudia wanachama wengi kuanzia wasanii wa muziki, waigizaji na viongozi mbalimbali kujitokeza kutaka nafasi za ubunge na udiwani.

Ni haki ya kila raia na mwanachama mwenye sifa za kuwania nafasi hizo kufanya hivyo, lakini swali tunalojiuliza ni sababu zipi zimefanya msululu wa wanachama wa CCM kujitokeza kwa wingi huo?

Je, ni demkorasia iliyopo ndani ya chama, kuondolowa kwa mfumo wa miungu watu ndani ya chama kulikokuwa kunawafanya wenye nacho ndio wanapata na wasiyo nacho hawapati hata kama wana sifa zinazokubalika ndani na nje ya chama?

Yote haya yanaweza kuwa ni maswali yenye majibu sahihi ndani yake kwa sababu siku moja kabla ya kuanza mchakato wa uchukuaji fomu ulioanza jana na utakaomalizika Ijumaa ya wiki hii.

Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM Taifa, Hamphrey Polepole, anaeleza kuwa baada ya kukamilika kwa mchakato wa kumpata mgombea urais Tanzania na Zanzibar uliomalizika mwishoni mwa wiki iliyopita, wamefanya mabadiliko katika katiba ya CCM ili kupanua wigo wa demokrasia.

Anasema mkutano mkuu wa kata ambao awali ulijumuisha watu wachache kwa sasa utakuwa na wajumbe wapya wanaoingia katika kikao hicho ambao pia ni wenyeviti wa mashina yote katika kata husika ambao wanajulikana, pia mabalozi nao watapiga kura za maoni.

Kwa upande wa ngazi ya jimbo au uwakilishi, wataanza na Mkutano Mkuu wa Jimbo ambao wagombea wote wataingia na wataeleza kwa nini wanataka kupewa dhamana ya uwakilishi na CCM kisha kamati za siasa za ngazi mbalimbali zitafuata utaratibu kwa kuweka mapendekezo mpaka kufikia Halmashauri Kuu ya Taifa itakayoamua jina moja.

**Yote haya yanaweza kuwa ni maswali yenye majibu sahihi ndani yake kwa sababu siku moja kabla ya kuanza mchakato wa uchukuaji fomu ulioanza jana na utakaomalizika Ijumaa ya wiki hii.**

Polepole anaeleza kuwa wamejifunza kutoka katika mchakato wa kupata ugombea wa urais walioufanya hivi karibuni. Anaeleza kuwa mchakato wa upigaji kura katika chama hicho utakuwa wa wazi ili kuepusha malalamiko. Hivyo, wanataka uchaguzi ndani ya chama hicho kuwa huru na haki.

Sambamba na hilo, Polepole anaeleza utaratibu wa mawasiliano ndani ya chama na kubainisha kuwa hivi karibuni wataeleza sehemu ambayo taarifa za uchaguzi zitapatikana.

Suala hili na kuweka wazi mchakato wa upigaji kura ni wazi kuwa utaondoa makundi ndani ya chama na kuwaleta pamoja wanachama mara baada ya kumpata mgombea ambaye atawakilisha jimbo au kata.

Tofauti na awali watiania waliokatwa walibaki na vinyongo vinavyowagawanya na mwisho kumalizia hasira zao kwa kuwapigia kura wagombea wa upinzani. "Bora tukose wote ndiyo ilikuwa kauli ya waliokosa. Ni wazi kuwa utaratibu wa mwaka huu, hautawaga wana-CCM." Anasema.

Akisoma kipengele cha kanuni ya uongozi wa maadili ya chama kwa upande wa haki za wanachama, Polepole anasema mwanachama atakuwa na haki ya kugombea nafasi yoyote ya uongozi endapo kugombea nafasi nyingi kuitasababisha kuzorota kwa uhai wa chama, hatateuliwa.

Aidha, anatahadharisha wagombea na watiania kuepuka vitendo vinavyokatazwa na chama kama kuweka mabango na kutumia vipeperushi kwa kuwa haviruhusiwi kwa sababu ni sawa na kuanza kampeni kabla ya wakati.

Licha ya CCM kuweka wazi kanuni na taratibu za kuwapata wagombea hawa ni muhimu kila aliyechukua fomu ya kuwania nafasi hiyo kuwa sehemu ya ushindani kuwa atambue kuna kukosa na kupata.

Kadhalika wanaopata watambue wazi kuwa ilikuwa ni lazima apatikane mmoja na wengine wajipange kwa ajili ya kukitafutia chama ushindi kwa maslahi ya wote.


# HABARI PICHANI



Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB, Dk. Charles Kimei, akitia saini kabla ya kuchukua fomu za kuwania ubunge katika Jimbo la Vunjo kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mhadhiri wa Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM), Kitivo cha Sheria, Dk. James Jesse (kulia), akipokea fomu ya kuwania kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM), kugombea ubunge Jimbo la Segerea, kutoka kwa katibu wa chama hicho, Wilaya ya Ilala, Iddi Mkowa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, Mwanaidi Mbishe, akimkabidhi fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea ubunge wa Jimbo la Siha, Wakili maarufu Tumsifu Kweka, katika ofisi za CCM wilayani humo, jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**



Katibu wa CCM Wilaya ya Chamwino, Evelyne Jordan (kushoto), akimkabidhi fomu Happines Mgongo ya kugombea ubunge Jimbo la Mtera Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Katibu Msaidizi wa CCM Wilaya ya Dodoma Mjini, Said Ngomboi (kushoto), akimkabidhi fomu Amos Msanjila ya kuomba kuchaguliwa na chama hicho kugombea Jimbo la Dodoma mjini kwa chama hicho. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mtera, kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Livingstone Lusinde, akipokea fomu ya kuomba kugombea nafasi hiyo kutoka kwa Katibu wa CCM Wilaya ya Chamwino, Evarline Jordan jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yatoa mamilioni ujenzi barabara Madaba

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

SERIKALI imetoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya lami kilometa moja katika Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) Halmashauri ya Madaba, Razaro Kitomari, alisema fedha hizo zinatumika kujenga barabara ya Kipingo-Lita.

Alisema mkataba wa mradi huo ni wa siku 180 na ulianza Aprili 7, mwaka huu na unatarajia kumalizika Oktoba 6, mwaka huu.

Alisema utekelezaji wa mradi huo hadi sasa ni zaidi ya asilimia 50 na kwamba lengo la TARURA ni kuhakikisha wanakamilisha ujenzi wa barabara hiyo kabla ya mkataba.

Meneja huyo alisema hadi sasa kazi inakwenda vizuri kwa kuwa vifaa vyote vinavyohitajika vipo katika eneo la mradi.

"Katika mwaka wa fedha wa 2019/20, Halmashauri ya Madaba ni miongoni mwa halmashauri 65 nchini ambazo zimepatiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi za viongozi katika programu ya maendeleo," alisema Kitomari.

Akizungumza mara baada ya kukagua mradi huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Ruvuma, Odo Mwisho, aliipongeza Halmashauri ya Madaba kwa kushirikiana na TARURA kutekeleza mradi huo ambao unakwenda kuondoa shida ya ubovu wa barabara hiyo.

Alitoa rai kwa TARURA kuhakikisha wanajenga barabara hiyo katika viwango ambavyo vitaiwezesha barabara kudumu kwa muda mrefu kwa kuwa serikali inatoa fedha za walipakodi ambazo zinatakiwa kutumika kulingana na thamani ya mradi uliotekelezwa.



Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Pwani, Alban Kihula (kulia), akifafanua jambo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe (katikati), kuhusu wanavyopima mita za maji kabla ya kwenda kwa watumiaji wa mwisho. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Tanzania yakunwa Ufaransa kusifu mapambano corona

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI ya Tanzania imeipongeza Ufaransa kwa kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli kupambana na virusi vya corona na kuonyesha mfano kwa nchi nyingine namna ya kupambana na virusi hivyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, alitoa pongezi hizo juzi usiku kwenye hafla ya Kumbukumbu ya Uhuru wa Ufaransa.

Zungu alisema Ufaransa imeifungua dunia na kuielezea kuwa Tanzania iko salama na hakuna tishio lolote la virusi vya corona ingawa virusi hivyo vipo.

"Ninaipongeza sana Ufaransa. Mmefanya kile ambacho Rais Magufuli amekuwa akikifanya na kukisisitiza. Tanzania tuliamua kufungua mipaka yetu na shughuli nyingine ziendelee na hiki ndicho ambacho Ufaransa wameamua kufanya, tazama hata hapa tulipo, hakuna waliovaa barakoa," alisema Zungu.

Vilevile, waziri huyo alisema kuwa tukio la juzi (kukutanisha mabalozi na wanadiplomasia mbalimbali kusherehekea Siku ya Ufaransa) ni la kwanza kwa mabalozi kukutana pamoja kwenye hafla tangu kulipuka kwa virusi vya corona mwishoni mwa mwaka jana.

"Tunaziomba nchi nyingine kupitia kwa mabalozi wake, waache mara moja kuziwekea vikwazo nchi nyingine kutokana na virusi vya corona, wafungue mipaka yao shughuli nyingine ziendelee," alisema Zungu.

Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, alipongeza Tanzania kwa namna walivyopambana na mlipuko wa virusi vya corona na kuahidi Ufaransa kuendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania kupambana na magonjwa ya mlipuko vikiwamo virusi hivyo.

Alisema janga la corona bado halijakwisha, lakini Ufaransa na Tanzania wataendelea kushirikiana na kuungana kwa ajili ya maendeleo ya nchi hizo mbili.


**GSP AUCTION MART**

P.o.Box 31088 Dar es Salaam
Tanzania, Tel: + 255 687 638679 +255 654 922892
Sinza Africasana near by sokoni Africasana Block No. 31
Email: gsp.recovering@gmail.com / gsp.recovering@outlook.com

**KUMB No. TATA/2020/DM/005**

**GSP AUCTION MART** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na kampuni ya ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED S.L.P 40780 Dar es salaam tunapenda kutangaza mnada wa hadhara wa kuuza Magari kwa njia ya mnada wa magari twaja hapo chini.Siku ya Alhamisi tarehe 30/07/2020 mnada utaanza Saa 5:00 kamili asubuhi katika yadi ya ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED iliyopo Dar es salaam vingunguti na Mwanza Sinai.

| CUSTOMER NAME | MODEL | VEH_NO | LOCATION |
|---|---|---|---|
| | | | |
| STELLA MAGOTI MWIGULU | LPO 10.2T/52 | T316 DRK | DAR ES SALAAM |
| JAMES ANTHONY MMASSY | LP 909 | T432 DPS | DAR ES SALAAM |
| LUSUBILO JOSEPH KAJANGE | LPK 813 | T791 DRD | MWANZA |
| MAJID AHMED IDD | Ultra Bus | T773 DQM | MWANZA |
| CHOCHO TOURS COMPANY LIMITED | LP 909 | T483 DNZ | DAR ES SALAAM |
| TWAHIL ABDALLAH MPULUJI | LPO 10.2T/52 | T167 DPU | DAR ES SALAAM |
| CONSTANTINO MLAGALA MSONJELA | LP 909 | T881 DNQ | MWANZA |
| CONSTANTINO MLAGALA MSONJELA | LP 909 | T487 DNR | DAR ES SALAAM |
| ELIAS DEBLO ELIA | LPO 10.2T/52 | T906 DPK | DAR ES SALAAM |
| DEOGRATIUS ORGENES LYMO | LP909 Bus | T813DQK | DAR ES SALAAM |
| SALVANUS JOHN CHIDOWE | LP909 Bus | T870 DPA | DAR ES SALAAM |

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.
5. Kwa yeyote atakayeharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:**
**GSP AUCTION MART PO BOX 310088 DAE ES SALAAM.**
**+255 654 922 892, +255 687 638 679**


# Ushirika watoa mil. 100/- za maendeleo

**Na Gideon Mwakanosya, MBINGA**

CHAMA cha Ushirika cha Msingi Kimuli katika Kijiji cha Utiri, Kata ya Utiri, wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma, kimetoa Sh. milioni 100 kwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika kata za Kitanda, Utiri na Kihangi Mahuka.

Hayo yalibainishwa na Meneja wa chama hicho,, Ernest Komba, wakati akisoma taarifa ya utendaji kazi wa chama hicho, wakati wa ziara ya kukagua shughuli za chama iliyofanywa na viongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika Mbinga (MBIFACU) na viongozi wa ushirika ngazi ya Mkoa wa Ruvuma.

Komba alisema fedha hizo zilizotolewa na Chama cha Kimuli, zilitokana na mapato ya premium na ziada za ndani na kusaidia ukarabati wa majengo ya taasisi za elimu na afya, zilizomo katika maeneo yanayohudumiwa na Chama cha Kimuli.

Aliitaja miradi iliyopewa fedha na chama hicho ni Zahanati ya Lipumba Sh. milioni 14, Zahanati ya Kitanda Sh. milioni 9.5, Zahanati ya Utiri Sh. milioni saba na Sekondari ya Ndela Sh. milioni 15.

Miradi mingine ni Sekondari ya Kihangi Mahuka Sh. milioni 13, Sekondari ya Luli Sh. milioni 2.5, Sekondari ya Ngwilizi Sh. milioni 1 na Shule za Msingi 10 zilizoko katika Kata ya Utiri na Kitanda, ambazo zimepewa milioni 26.

Amesema awali wananchi walikuwa wakichangia fedha za mifukoni, au kusubiri miradi itekelezwe na Serikali. Lakini kwa sasa Chama kimeona ni vema kufanya maendeleo hayo ili kurudisha fadhila kwa wananchi ambao huuza mazao katika chama cha msingi ambapo hivi sasa wananchi wanaona faida ya uwepo wa chama cha Ushirika cha Msingi Kimuli.

"Chama kimetoa faida yake kwa kuchangia utekelezaji wa miradi mbalimbali, ya afya na elimu kwa kuchangia ukarabati na ujenzi wa madarasa kutokana na uhitaji wa taasisi husika, ili kuamsha ari kwa jamii na watambue umuhimu wa chama chao cha ushirika," alisema na kuongeza:

"Kwa kuwa kama sio chama kutoa kiasi hicho basi wangelazimika kuchangia au kusubiri Serikali itoe fedha za kutekeleza miradi hiyo ya maendeleo."

Komba ametoa rai kwa Wananchi wa kata zilizo katika mradi huo wajiunge na Chama cha ushirika na Msingi Kimuli kwa maendeleo ya kaya na jamii kwa ujumla. Kaimu Meneja wa MBIFACU, Henerck Ndimbo, alimpongeza Rais John Magufuli kwa kuviongezea nguvu vyama vya ushirika na msingi kwa kuwa kwa sasa wakulima wengi baada ya kupata elimu ya ushirika wanauza mazao yao kupitia vyama vya ushirika na kupata manufaa mengi.

Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Ruvuma, Bumi Masuba, aliipongeza MBIFACU kwa kusimamia vema vyama vya msingi hali ambayo imewezesha kuimarisha ushirika.

## HABARI KITAIFA

# Mchanga sasa kuanza kusafirishwa saa 24

**Na Yasmine Protace, MKURANGA**

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Filbeto Sanga, amesema kuwa utaratibu wa kusafirisha mchanga kwa saa 24 unaandaliwa.

Amesema baada ya maandalizi kukamilika, wataruhusiwa kusafirisha kwa saa 24 badala ya muda wa sasa wa saa 12.

Sanga aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wadau wa mchanga, ambao wanachimba mchanga katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

"Utaratibu umeishaandaliwa na mkuu wa mkoa wa Pwani, wa kusafirisha mchanga saa 24, badala ya saa 12," alisema.

Aliongeza kuwa kusitishwa kusafirisha mchanga kwa saa 24 kulitokana na ajali iliyotokea mwaka juzi na kuua watu 14 wa familia moja.

Alisema Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, atatoa kibali siku yoyote kuanzia sasa ambacho kitawaruhusu wadau wa mchanga kusafirisha kwa saa 24.

Sanga akiongeza kuwa pamoja na kuruhusiwa kusafirisha mchanga, wenye magari watatakiwa kuwaajiri madereva wenye sifa kwa ajili ya shughuli hiyo.

Alisema kutokana na kusafirisha mchanga kwa saa 24 wamiliki wa malori wanatakiwa kuajiri madereva wawili.

**Alisema Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, atatoa kibali siku yoyote kuanzia sasa ambacho kitawaruhusu wadau wa mchanga kusafirisha kwa saa 24.**

# Taasisi zinazosimamia wajasiriamali zatakiwa uwekezaji katika TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeziagiza taasisi na mamlaka mbalimbali zinazosimamia ustawi wa wajasiriamali nchini kuwekeza zaidi kwenye teknolojia ya habari na mawasilano (TEHAMA).

Imeelezwa kuwa hatua hiyo itasaidia upatikanaji taarifa za uhakika kuhusu bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali hao ili waweze kupata masoko ya uhakika kutoka ndani na nje ya nchi.

Akizungumza wakati wa hafla ya kuhitimisha Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya jijini Dar es Salaam -Sabasaba, Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar, Balozi Amina Salum Ali, alisema uwapo wa taarifa za uhakika kuhusu uzalishaji na masoko utawasaidia sana wajasiriamali wakiwamo wakulima na wafanyabiashara ambao wanahitaji taarifa hizo muhimu ili waweze kuuza na kununua mazao yao kwa wakati sahihi.

"Zaidi pia mamlaka hizi hususani Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade) mna wajibu wa kuhakikisha mfumo wa utendaji wenu unaanzia chini kabisa ili muweze kuwafikia wazalishaji huko walipo si tu muwasaidie kuwaunganisha na masoko bali pia muweze kufahamu haswa changamoto zinazowakabili ili ziwasilishwe serikalini kwa wakati," aliongeza.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bushungwa , Katibu Mkuu Wizara hiyo, Prof. Riziki Shemdoe, alisema wizara hiyo kupitia TanTrade inaendelea kuyaboresha maonyesho hayo, huku akizipongeza taasisi mbalimbali ikiwamo Benki ya NBC Tanzania ambayo ndio mdhamini mkuu wa maonyesho hayo na pia ikiwa mstari wa mbele kusimamia ustawi wa wajasiriamali nchini.

"Lengo ni kuhakikisha maonyesho haya yanafanyika katika ubora wa kimataifa na yanatimiza malengo ya kuanzishwa kwake kwa maana haswa ya kuwasaidia wafanyabiashara waweze kukutana na kubadilishana fursa za kibiashara na hili litafanikiwa zaidi kupitia wingi wa washiriki kwenye maonyesho haya," alisema.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo ya kutambua mchango wa Benki ya NBC katika kufanikisha maonyesho hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Theobald Sabi, alisema wamekuwa wakiyapa uzito maonyesho hayo kwa kuwa yamekuwa yakiwakutanisha wajasiriamali kutoka kila kona ya nchini, hivyo kwenda sambamba na hitaji la msingi la benki hiyo iliyojikita zaidi katika kutoa huduma zinazokwenda sambamba na mahitaji wa wajasiriamali nchini.

"Popote walipo wajasiriamali ni wazi pia Benki ya NBC tutakuwapo," alisisitiza huku akibainisha kuwa benki hiyo imejipambanua kama kituo kimoja chenye mahitaji yote ya wajasiriamali kwa kutoa huduma mahususi na maalum zinazoakisi mazingira ya biashara ya ndani kwa lengo la kukuza na kuendeleza sekta ya wajasiriamali nchini.

"Katika kuhakikisha hilo, uwapo wetu kwenye maonyesho haya ulikuwa sambamba na wajasiriamali kupitia klabu ya biashara inachoitwa 'NBC-Club' ambayo inawaunganisha wajasiriamali na kuwawezesha kufanya safari za kibiashara, huduma za bure za ushauri wa kibiashara na upendeleo maalum katika baadhi ya huduma, hatua ambayo inalenga kuleta mabadiliko katika sekta hii muhimu," alisema.

Utafiti unaonyesha kuwa sekta ya wajasiriamali inachangia asilimia 35 ya Pato la Taifa (GDP) huku ikiajiri zaidi ya watu milioni 5.2 nchini. Hata hivyo sekta hiyo imekuwa ikikabiliwa na vikwazo kadhaa ikiwamo ufikiwaji mdogo wa huduma za kifedha, sababu iliyotajwa kuwa ndio iliyopelekea benki hiyo kuwekeza zaidi katika sekta hiyo ikilenga kuwasaidia kuboresha mazingira ya biashara kwa kutoa huduma mahususi kwa ajili yao.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya TANTRADE, Dk. Ng'waza Soko, alisema licha ya changamoto ya ugonjwa wa COVID-19 iliyoikumba nchi na dunia kwa ujumla, maonyesho hayo kwa mwaka huu yamefanikiwa kuvunja rekodi wa idadi ya watu waliotembelea viwanja hivyo kutoka 53,504 wa mwaka jana hadi 57,608 wa mwaka huu ikiwa niongezeko la watu zaidi ya 4,000.



Waziri wa Viwanda na Biashara Zanzibar, Balozi Amina Salum Ali (kulia), akikabidhi Tuzo ya Banda Bora katika Sekta ya Mawasiliano na TEHAMA kwa Meneja Mauzo wa Vodacom Tanzania PLC, Kanda ya Temeke, Angetile Martin, baada ya kampuni hiyo kuwa mshindi wa kwanza katika kipengele hicho, wakati wa Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, yaliyomalizika juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utoaji huduma hospitali ya wilaya waanza

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

HOSPITALI ya Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara ambayo imejengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.5, ilianza kutoa huduma rasmi jana kwa wakazi wa wilaya hiyo.

Ufunguzi huo ulifanyika katika kijiji cha Mbuyuni Kata ya Mbuyuni ambapo imejengwa na hafla hiyo kuhudhuriwa na na mamia ya wananchi wa wilaya hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Changwa Mkwazu, alisema kuanza kwa utoaji wa huduma hizo kwa wananchi utakuwa ni mkombozi kwao.

Alisema Rais John Magufuli alitoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya ujenzi, lengo likiwa kupanua wigo wa utoaji wa huduma za afya kwa wakazi wa Masasi hasa waliopo pembezoni mwa wilaya hiyo ambao hutembea umbali mrefu hadi Masasi kutafuta huduma hizo katika Hospitali ya Mkomaindo.

Mkwazu alisema hospitali hiyo ina majengo saba ambayo yameanza kutoa huduma hizo kwa sasa, lakini matarajio ni kuwa na jumla ya majengo 22 hadi kukamilika kwake.

"Hatujui Rais Magufuli tutampa nini kwa kuamua kutupatia fedha hizi kwa ajili ya kujenga majengo 22 ya hospitali hili... tumpongeze kwa jambo hili na sasa huduma zimeanza kutolewa kwa wananchi ni jambo la furaha," alisema Mkwazu.

Alisema serikali imeamua kutoa fedha hizo kwa lengo la kuendelea kupanua wigo wake wa utoaji huduma za afya nchini hasa katika maeneo ya wilaya ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Aidha, serikali imeipatia halmashauri hiyo kiasi kingine cha Sh. milioni 300 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya maji na umeme katika hospitali hiyo, hivyo wananchi waendelee kutoa ushirikiano katika kukamilisha hospitali ili iweze kutoa huduma kama ilivyokusudiwa. Mkwazu alisema serikali itaendelea kuwajali wananchi wa Wilaya ya Masasi kwa kuwapatia huduma mbalimbali za maendelea zikiwamo za afya, miundombinu mingine kama barabara, maji, umeme, hivyo wananchi waendelee kuwa na imani na serikali.

Mganga mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Abdul Rashid, alisema huduma ambazo zitaanza kutolewa katika hospitali hiyo ni za wagonjwa wa nje (OPD) za uzazi.

Zingine ni za maabara, ustawi wa jamii, kitengo cha dawa na kitengo cha maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Alisema anawataka watoa huduma katika hospitali hiyo kufuata maadili ya kazi yao kwa kufanya kazi karibu na wananchi na ushirikiano ili kuondoa malalamiko yasiyo ya msingi.

# SBL yapanua sasa viwanda vyake

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya vikwazo kwa biashara nyingi duniani kutokana na ugonjwa wa corona, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) imesema kusimama imara na kuendelea katika uzalishaji.

Kampuni hiyo imesema imeweza kukamilisha upanuzi wa kiwanda chake cha bia cha Dar es Salaam uliogharimu paundi za Uingereza milioni 10 (sawa na shilingi bilioni 30), huku upanuzi wa kiwanda chake cha Moshi ukiwa unaendelea kwa gharama ya Paundi za Uingereza milioni 4.5 (sawa na Shilingi bilioni 13.5).

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, uwekezaji huo mkubwa umechangiwa kwa kiasi kikubwa na mazingira mazuri ya biashara ambayo pia yamesababisha kukua kwa soko la bia nchini.

"Tulitoa ahadi kwa wateja wetu kuwa kama mahitaji yataongezeka, tutawekeza katika kupanua uzalishaji ndani ya miaka michache ijayo na ndicho ambacho tumekifanya na tunachoendelea kukifanya," Ocitti alisema.

Alisema upanuzi huo wa uzalishaji umekwenda sambamba na ongezeko la kodi ambalo kampuni hiyo imelipa kwa Serikali. Mwaka jana SBL ililipa shilingi bilioni 132 kama kodi ikiwa ni ongezeko la asilimia 10 kutoka shilingi bilioni 121 iliyolipwa mwaka 2018.

Ukuaji wa kampuni hiyo kwa mujibu wa mkurugenzi wake mtendaji, umewezesha kuongezeka kwa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja ambapo kwa sasa zaidi ya watu 800 wameajiriwa na kampuni hiyo.

Alisema wakulima wanaozalisha shayiri, mtama na mahindi mazao ambayo hutumiwa na kampuni hiyo kuzalisha bia ni kundi lingine ambalo linanufaika na upanuzi. SBL ilinunua zaidi ya tani za ujazo 17,000 za nafaka kutoka kwa wakulima wa ndani sawa na asilimia 70 ya mahitaji yake yote ya malighafi katika kipindi cha mwaka jana.

"Lengo letu ni kuongeza kiasi cha malighafi tunazonunua kutoka kwa wakulima wa ndani na kufikia asilimia 85 ya kiwango kinachotakiwa kwa uzalishaji wa bia kufikia mwaka 2022, jambo ambalo litawahakikishia wakulima uhakika wa soko kwa mazao yao," aliongeza.

**"Tulitoa ahadi kwa wateja wetu kuwa kama mahitaji yataongezeka, tutawekeza katika kupanua uzalishaji ndani ya miaka michache ijayo na ndicho ambacho tumekifanya na tunachoendelea kukifanya," Ocitti alisema.**

# Wakulima waonyeshwa fursa miti ya mitiki

**Na Stevie Chindiye, NYASA**

IMEELEZWA kuwa hekari moja ya miti aina ya mitiki inaweza kumwingizia mkulima zaidi ya Sh. milioni 400 na kujiletea manufaa ya kujiimarisha kiuchumi.

Hayo yalisemwa na Ofisa wa Maliasili wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma, Bagingo Bugingo, alipokuwa akizungumza na wanahabari na wakulima wanaotekeleza mradi wa kupanda miti kibiashara.

Hamasa hiyo inatokana na halmashauri hiyo kuweka lengo la kupanda miti hekari 1,750.

Bugingo alisema kuwa katika harakati za kufika malengo hayo, hadi sasa wilaya hiyo imeshapanda miti katika eneo la hekari 317.5 na miti yote inaendelea vizuri.

Alisema hata hivyo, wakulima wengi katika mwambao mwa Ziwa Nyasa wanakata tamaa ya kuendelea kupanda miti hiyo ambayo tangu kupandwa hadi kuvunwa inachukua kati ya miaka 15 hadi 20.

Alisema mradi wa pandamiti kibiashara unatekelezwa katika safu ya Milima ya Livingstone katika kata za Lipingo, Liuli, na Kihagara Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma na kwamba unaendelea kwa kiwango cha kuridhisha.

Naye Mratibu wa Mradi wa Forvac Mkoa wa Ruvuma, Marcel Mtunda, akikagua mradi wa panda miti kibiashara unaotekelezwa katika Kijiji cha Mkali 'A' na Kijiji cha Nkalachi Kata ya Liuli, na kwamba ameridhishwa na maendeleo ya ukuaji wa miti, na kuwaomba wananchi wapalilie miti hiyo ili isiungue kwa moto.

Alisema wananchi baada ya kupata elimu ya upandaji miti kibiashara, wamehamasika na kupanda miti ambapo amesema mradi huo utawanufaisha wakulima wa miti katika vijiji hivyo kwa kuinua hali ya maisha na kuongeza kipato katika ngazi ya familia.

Rais wa Shirikisho la Viwanja vya Misitu Tanzania (SHIVIMITA), Ben Mfungo, alisema tangu mwaka 1988 mahitaji ya soko la miti aina ya mitiki limekuwa likiendelea kukua ndani na nje ya nchi.

"Juzi tu nilikuwa Accra nchini Ghana, tulijulishwa kwamba Jumuiya ya ECOWAS ilichukua mbegu za miti ya mitiki toka Tanzania baada ya kubainika mbegu za Tanzania zina ubora zaidi katika soko la dunia, hivyo nao wameamua kuchukua mbegu hiyo inayokidhi soko la kimataifa," alisema Mfungo.

Kufutia hali hiyo aliwataka wakulima wapya wa mitiki katika Wilaya ya Nyasa na maeneo mengine ambayo zao hilo linaweza kustawi, waongeze uzalishaji wa mitiki kwa sababu mahitaji yake yanaendelea kuongezeka.

"Mahitaji ya mti huu katika soko la duniani ni makubwa, ndiyo maana nchi za Ulaya na za Asia zikiongozwa na China na India wananunua miti aina ya mitiki kwa wingi kutoka Tanzania na hatujaweza kufikisha hata robo ya mahitaji yao," alibainisha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wiaya ya Nyasa, Jimson Mhagama, aliwashauri wananchi na kampuni za wawekezaji wanaohitaji kuwekeza katika sekta ya misitu wafikie katika wilayani Nyasa kuwekeza kwenye ardhi yenye rutuba.

Mshauri wa Misitu katika Mradi wa Panda Miti Kibiashara, Sangito Sumari, alisema katika Wilaya ya Nyasa mradi huu unahusu miti aina ya mitiki ambayo utafiti umebaini inastawi vizuri katika hali ya hewa iliyopo mwambao mwa Ziwa Nyasa.



Baadhi ya wakazi wa Kitongoji cha Karuenyi Kijiji cha Mikuyu, Kata ya Nyamrandirira, Musoma Vijijini mkoani Mara, wakishirikiana na mafundi kujenga darasa la shule ya awali juzi, ili kuwapunguzia kutembea umbali mrefu kufuata elimu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kigwangalla ataka tahadhari corona JNIA

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, amewataka watumishi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA), kuongeza nguvu ya kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona.

Kadhalika, amewataka kuhakikisha kwamba wanaweka mazingira yanayohakikisha usalama kwa wageni wanaoingia nchini.

Dk. Kigwangalla alisema kuongeza nguvu katika kuchukua tahadhari hiyo kutasaidia kuendelea kuiweka Tanzania kuwa salama na pia kuiweka katika taswira nzuri kimataifa na kuongeza uwezekano wa watalii kuvutiwa kuja nchini.

Dk. Kigwangalla alitoa wito huo katika ufunguzi wa wafanyakazi wa uwanja huo Dar es Salaam.

Alisema ni jambo jema kwa Tanzania kufungua milango kwa wageni kuingia nchini, lakini kuna haja ya kuandaa mazingira kuwa katika hali ya usalama zaidi.

"Kuchukua tahadhari siyo tu kwa faida yetu, lakini kwa wale wageni wanaoendelea kuja nchini kwetu, kama wakitukuta hatuchukui hizo hatua kwa sababu sisi tuko salama wanaweza wakaenda kuichafua taswira ya nchi yetu na watu wakaogopa kuja Tanzania," alisema Dk. Kigwangalla.

"Kwa hiyo sisi tulio katika mnyororo huu tuwe kama makini na tunapompitisha au kumkaribisha mgeni aone kwamba Tanzania ni salama na ili tuwavutie watu wengine."

Dk. Kigwangala alisema kufungua anga kunatakiwa kuendane na utayari wa wenyeji kuchukua tahadhari zote ambazo zinatakiwa na siyo kuridhika na hali iliyopo.

"Mpango wa kufungua anga lazima uwe na utayari wa kuwapokea wageni, wakute tumejiandaa kuchukua tahadhari kwa nguvu zote alisema," alisema Waziri Kigwangalla.

# Fursa kuwabana wagombea si kampeni za kushangilia tu



Ukurasa 12



Ukurasa 13

## Wasudan Kusini ‘washerehekea’ milio ya risasi, simanzi na vifo

siasa

JUMATANO JULAI 15, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# Dokta Shein, mwenza aliyeaminiwa na Mkapa

**Na Mashaka Mgeta**

MIAKA 10 ya utawala wa Rais Ali Mohamed Shein, kuiongoza Zanzibar, inafikia ukingoni mara baada uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Maandiko mbalimbali vikiwemo vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi, vinamtaja Dk Shein kama mwanasiasa aliyeonyesha kipaji cha uongozi tangu akiwa kijana.

Anatajwa kupitia nafasi mbalimbali za uongozi, lakini kwa sehemu kubwa, ni kuibuliwa kwake na Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, kuwa Makamu wa Rais Julai 12, mwaka 2001, kulikomfanya Shein kujulikana zaidi kwa walio wengi.

Juni 12, 2001, Mkapa alimteua Dk Shein kushika wadhifa huo na siku iliyofuata, yaani Juni 13, 2001, akaliwasilisha jina lake bungeni ambako wabunge walilipitisha kwa kuiidhinisha kwa kura nyingi.

### KUONDOKA DK OMAR

Uteuzi huo ulitokana na kifo cha aliyekuwa mtangulizi wake, Dk Omar Ali Juma , aliyefariki Julai 4, 2001 na kuibua mshtuko nchini na kwingineko Afrika.

Rais wa wakati huo, Mkapa, aliutangazia umma na kuripotiwa na vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo vyombo vya kimataifa, Julai 5, mwaka 2001 kuwa Dk. Omar wakati huo akiwa na miaka 60 amefariki duniani kutokana na ugonjwa wa moyo.

Rais Mkapa alinukuliwa akitangaza kifo cha makamu wake wakati huo aliyefariki saa 5:45 usiku na alitangaza siku saba za maombolezo ya kifo hicho.

Dk. Omar aliaminika kuwa kiongozi aliyekubalika kwa karibu na Mkapa. Alishika wadhifa huo tangu walipoingia madarakani mwishoni mwa mwaka 1995.

Mkapa alimtaja Dk Omar kama msaidizi wake wa karibu, mtu mwenye thamani, mchapakazi na asiyekuwa na makuu aliyeacha pengo kubwa kwa taifa

### UTEUZI WA SHEIN

Ni jambo lililotarajiwa kutokana na mtizamo huo wa kiwasifu, uteuzi wa mrithi wa Dk. Omar, angepatikana kiongozi mwenye kaliba hiyo,



Rais mstaafu Ben Mkapa na Rais wa SMZ anayemaliza muda wake, Dk. Ali Mohamed Shein , katika harakati za kisiasa. **PICHA: MTANDAO**

hapo ndipo alipoibuliwa Dk. Shein, akitokea kwenye safu ya Baraza la Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

Dk. Shein , ambaye kitaaluma anaangukia fani ya utabibu wa binadamu, mwishoni mwa wiki iliyopita katika vikao vya CCM vya kumpitisha mrithi wake jijini Dodoma, alijitambulisha kuwa na miaka 72 na kuitumikia SMZ tangu mwaka 1969.

Hakuonekana sana katika ngazi za juu kiutendaji serikalini, hadi pale alipoibuliwa kutumika kama naibu waziri ndani ya SMZ. Kitaaluma, elimu yake ya juu aliipata kutoka Chuo Kikuu cha Odessa nchini Urusi na pia kupata elimu zaidi Uingereza.

Anatajwa kuonyesha umahiri wa uongozi tangu alipokuwa kijana hasa baada ya kujiunga na Umoja wa Vijana wa Afro-Shirazi (ASP) wakati akiwa mwanafunzi .

Mmoja wa watu waliowahi kusoma na Dk Shein katika Shule ya Lumumba huko Zanzibar, Dk Mohammed Saleh Jidawy, alikaririwa na vyombo vya habari akitaja wasifu wake mwingine kuwa mwanariadha hodari, katika ujana wake.

Pia, katika zama hizo za ujana anatajwa kujitolea katika shughuli za kijamii za kuwaelimisha vijana wenzake kujitambua na ndani ya siasa za ASP, anatajwa kuwanoa wenzake kwenye ulingo wa siasa za mwelekeo wa chama chao.

Mwaka 1997, alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM - NEC na kutokana na nafasi hiyo, aliteuliwa kwenye Kamati Kuu ya CCM mwaka 2005.

### KUINGIA IKULU

Dk. Shein alishinda uwakilishi katika jimbo la Mkanyageni katika uchaguzi mkuu wa Novemba 2000 na kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Baada ya ushindi huo, aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba na Utawala Bora, Novemba 2000. Wakati wa kinyang'anyiro cha uchaguzi mkuu wa 2005, Dk Shein aliteuliwa kuwa mgombea mwenza kupitia CCM. Wakati huo, mgombea urais kupitia chama hicho alikuwa Jakaya Kikwete.

Annet Ngahyoma, mmoja wa watu waliofanya kazi na Dk Shein baada ya kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais, ananukuliwa na vyombo vya habari akisema kuwa kiongozi huyo ni mtu mpole na mwenye kupenda dini.

### URAIS WA Z'BAR

Dk Shein aliongoza baada ya kushinda uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka 2010 na kuchukua hatamu za uongozi. Ilikuwa ni baada ya Rais Amani Karume, aliyekuwepo madaraka, kumaliza kipindi chake cha uongozi.

Shein aliapishwa Novemba 3 mwaka 2010 na kuanza kazi na hata leo anajulikana pia kuwa ni mtu mwenye msimamo, asiyeyumbishwa katika kile anachokiamini.

Mwaka 2015, Dk Shein aliwania urais kwa mara ya pili kukamilisha kipindi cha miaka 10 ya urais wa Zanzibar, lakini akiwa ametumikia takribani miaka tisa ya jukumu la Makamu wa Rais wa Muungano.

Baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu, Dk Shein atastaafu kwa mujibu wa katiba , akiwa ni kiongozi aliyedumu madarakani kwa muda mrefu akizitumikia Serikali ya Muungano na ya Mapinduzi ya Zanzibar.

KUELEKEA UCHAGUZI MKUU

# Fursa kuwabana wagombea si kampeni za kushangilia tu



Wapigakura wakijiandikisha kwenye moja ya uchaguzi uliowahi kufanyika nchini. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

KIVUMBI cha uchaguzi mkuu kinaanza kutimka rasmi kwa wagombea udiwani na ubunge, baada ya pazia la kuchukua fomu kufunguliwa kuanzia jana.

Mchakato huo unawahusu wagombea wa CCM pekee na kwa vyama vingine uchukauaji ulishaanza.

Wakati huo pilikapilika zikipamba moto wagombea kutoka vyama mbalimbali vya siasa wakiwa na fomu za kuwania urais ubunge na udiwani, ndiyo wakati wa wapiga kura kuwatafakarisha.

Mchakato wa kufanikisha uchaguzi huo unapoendelea , ndiyo wasaa kwa Watanzania hasa wapigakura kutambua mambo ambayo yatasaidia kuwapata viongozi watakaowaletea maendeleo na kuwaondolea umaskini.

Kwanza ieleweke kuwa uchaguzi ni kiwango cha juu cha uwajibikaji wa kisiasa na ndiyo wakati ambao wanasiasa hutumia miezi kadhaa kufanya kampeni kujaribu kuwashawishi wananchi ili wawachague.

Hivyo ni muhimu wapigakura kuwa makini katika kuchagua wagombea, kwani ni wakati ambao wanakuja na ahadi tamu za kuwashawishi na kuwaahidi kuwaletea maendeleo lakini wengi wanashindwa kutekeleza walichoahidi kwenye kampeni.

> Ni ajabu kulalamikia shule kukosa vyoo bora, jiko la kupikia chakula cha wanafunzi na hata ofisi za kijiji kukosa vyoo wakati kuna fedha za mfuko huo.

**KUANZA KUHOJIANA**

Ni wakati sasa kwa wapigakura kuwahoji wagombea katika kampeni, siyo kushangilia tu pale wanapoahidiwa jambo fulani na bila kutafakari au kuuliza jinsi ambavyo mhusika atalitekeleza.

Kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi, katika majimbo mbalimbali kwamba, wabunge wao hawaonekani majimboni kwa muda mrefu na hawajatimiza ahadi.

Ni mambo waliyoahidiwa wakati wa kampeni. Hata kwenye rasimu ya katiba mpya, wananchi walipendekeza kipengele cha wapigakura wawe na mamlaka ya kumuwajibisha kwa kumkataa mbunge ambaye hajaonekana kwa muda mrefu jimboni.

Lakini mapendekezo hayo yalikwama kwenye Bunge Maalumu la Katiba, hivyo ni wajibu wa wapigakura wenyewe kujipanga vizuri na kuhakikisha wanapata wabunge au madiwani wenye ahadi zinazotekelezeka.

Katika kampeni za uchaguzi, yapo mambo kadhaa, ambayo wapigakura na wananchi kwa ujumla wanatakiwa kuyatilia maanani kama vigezo vya kuwapigia kura wagombea.

Kuna baadhi ya masuala ya msingi kama afya, elimu na maji, miundombinu, nishati na usalama, hivyo vyote wanasiasa hucheza navyo kwa ahadi kemkem na kushangiliwa na wapigakura, lakini mwisho wake hakuna utekelezaji.

Kwa mfano, mgombea anawaahidi wapigakura kwamba, atawaletea maji, wanatakiwa kumhoji ili atayafikishaje jimboni hapo? Kwa fungu gani? Wambane aweke wazi mikakati yake ya kuwaletea huduma hiyo, ili waridhike nazo kuliko kushangilia ahadi hewa.

Mazoea ya aina hiyo yamesababisha wagombea kuendelea kuahidi hata vitu, ambavyo hawana uwezo navyo, ili mradi tu wapate kura kwa ajili ya kufanikisha mambo yao binafsi.

Uchaguzi wa mwaka huu uwe ni wa wapigakura kuwabana wagombea ili pale wasiporidhika na maelezo yao, basi wafanye uamuzi mwingine kuliko kuendelea kukumbatia viongozi wasio na nia ya kuwaletea maendeleo.

Yapo mambo mengi ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi kwa ajili ya maendeleo ya taifa, wapigakura ni vyema wasikie wagombea wana mikakati gani katika kukabiliana nayo.

**FADHILA YA VIJISENTI**

Wapo baadhi ya wapigakura wanaoamini kwamba, mtu anapochaguliwa kuwa mbunge, basi ni wakati wa kwenda kupata pesa ambazo na wao watakuwa wanapewa kila wanapomuomba kiongozi wao.

Wanaamini kuwa kwa vile wamempigia kura anawajibika kuwanunulia 'chai na vitumbua'

Lakini ukweli ni kwamba, jukumu la mbunge ni kuhamasisha na kushirikiana na wananchi kuleta maendeleo na siyo kuwa mfadhili wa jimbo kama, ambavyo baadhi ya wapigakura wanadhani.

Wananchi wakimchagua mbunge mwenye nia ya dhati ya kuwaongoza, atakuwa mwepesi kuwashirikisha katika uibuaji wa miradi ya maendeleo na kuweka mikakati ya kuiendeleza.

Kimsingi mbunge au diwani, ni watu wa kutia msukumo kwenye serikali ya iharakishe huduma zinazohitajika kwenye maeneo yao, si kwamba wanatoa pesa mfuko kuleta maendeleo.

Hata hivyo mbunge anawajibika kuleta mabadiliko ya hali za wananchi kwenye maeneo yao kwa kushirikiana kutatua kero zilizo kwenye uwezo wao.

Vilevile bado viongozi hao wana nafasi ya kuhamasisha wananchi kuchangia maendeleo kwenye majimbo na kata zao, huku nao wakishiriki kwa kutoa michango yao na siyo kusubiri kuchangia pesa kwenye misiba.

**DHANA MUHIMU**

Watanzania wanakumhushwa mara kwa mara na Rais John Magufuli, kwamba, maendeleo hayana chama, hivyo hata katika kampeni, ni vyema wakazingatia hilo wanaposikiliza sera za wagombea bila kuangalia vyama wanavyotoka.

Yawezekana mgombea anayefaa anatokea chama ambacho sicho cha mpigakura, lakini kwa sababu ana uwezo wa kuleta maendeleo, basi achaguliwe ili aongoze.

Lakini jambo la msingi ni kupima ahadi za wagombea wote na kuhoji jinsi watakavyozitekeleza ili iwe rahisi kuchagua wanaofaa kusimamia maendeleo na kuondoa umaskini.

Ikumbukwe kwamba, mbali na kuhamasisha shughuli za maendeleo majimboni, wabunge pia ni wenyeviti wa fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo, ambao wakiusimamia kikamilifu unaweza kuinua maeneo yao.

Huo ni mfuko wa kuchochea maendeleo ya jimbo ulioanzishwa mwaka 2009 kwa Sheria Namba 16 ya mwaka 2009 iliyotungwa na Bunge, ambapo fedha hizo hutolewa katika majimbo yote ya uchaguzi Bara na Zanzibar.

Vigezo vinavyotumika kugawa fedha za mfuko huo ni idadi ya watu asilimia 45 na huingizwa moja kwa moja katika akaunti za halmashauri na zinasimamiwa kwa taratibu za Sheria ya Fedha.

Wananchi wawe na 'jeuri' ya kuhoji na kufuatilia matumizi ya mfuko wa fedha za maendeleo ya jimbo badala ya kulalamika kwa viongozi wakuu hasa Rais, Waziri Mkuu na watendaji wa chama kuwa hawana baadhi ya huduma.

Ni ajabu kulalamikia shule kukosa vyoo bora, jiko la kupikia chakula cha wanafunzi na hata ofisi za kijiji kukosa vyoo wakati kuna fedha za mfuko huo.

Kuhoji matumizi ya fedha za umma ni wajibu wa kila mmoja kwa kuwa pesa hizo ni za Watanzania wote walipakodi na wazalishaji, viwandani, mashambani, migodini, kwenye kilimo na ufugaji.

MIAKA 9 YA UHURU

# Wasudan Kusini 'washerehekea' milio ya risasi, simanzi na vifo



Maelfu ya wakimbizi wa ndani waliokusanyika katika eneo la kanisa la Emmanuel huko Yei, Sudan Kusini. **PICHA: UN**

JULAI mwaka huu inatimia miaka tisa tangu Sudan Kusini, taifa changa kiumri duniani lijinyakulie uhuru baada ya kujitenga na Sudan iliyokuwa inaongozwa na Omar al-Bashir.

Lakini, tangu kupata uhuru taifa hilo linachokishuhudia ndani ya muongo mmoja ni vita zaidi. Hakuna amani, raia wake wamekuwa sehemu ya wimbi kubwa la wakimbizi na mahangaiko.

Pamoja na madhila hayo sasa nchi hiyo inapambana na janga la corona kwa kuwaepusha wakimbizi na ugonjwa huo , kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR).

Katika mji wa Ajuong Thok huko Sudan Kusini wafanyakazi wa UNHCR wakishirikiana na serikali na wadau wengine wa misaada kudhibiti kusambaa kwa janga la COVID-19.

Taifa hili changa duniani Alhamisi Julai 9 lilisherehekea uhuru wake huku likiendelea taratibu kujikwamua kutoka kwenye vita vya wenyewe kwa wenye baada ya kuanzishwa kwa serikali ya mseto Januari mwaka huu 2020, lakini katika baadhi ya maeneo kwa mujibu wa UNHCR vita bado vinaendelea na kutishia juhudi kubwa zilizopigwa kuelekea amani ya kudumu.

Licha ya kutiwa saini kwa mkataba wa amani mwaka 2018 na kuanzishwa kwa serikali ya mseto juhudi zaidi zinahitajika kuhakikisha kila kona ya nchi hiyo inakuwa na amani kwa mujibu wa UNHCR na kuongeza kuwa sasa janga la corona limekuwa tishio jipya hasa.

Kuna wakimbizi wa ndani zaidi ya milioni 1.7 ambao wanahitaji ulinzi si tu dhidi ya machafuko bali pia maambukizo na maangamizo ya COVID-19.

> “Hakuna amani, watoto wangu wawili wamezaliwa vitani. Sijui jinsi gani serikali itawasaidia kukua bila milio ya risasi. Vita vimeathiri akili zao na wamekuwa kama wendawazimu.

UNHCR na wadau wengine wa misaada ya binadamu wanafanya kila wawezalo kuwalinda wakimbizi hao wa ndani dhidi ya corona na wale walio nje ya nchi zaidi ya 300,000.

Ingawa kuna matumaini, shirika hilo linatoa wito kwa viongozi wa Sudan Kusini kuongeza kasi ya kufikia amani ya kudumu ya kumaliza mgogoro mkubwa zaidi duniani wa wakimbizi wa ndani na watu waliotawanywa.

### HISTORIA YA KUJITENGA

Sudan Kusini ilijipatia uhuru wake kutoka Sudan ya al-Bashir Julai 9, 2011 kufuatia kura ya maoni ambayo asilimia 80 ya watu walipiga kura ya ndiyo ya kujitenga.

Lakini tangu kujitenga huko hawajapata amani. Mathalani, katika kambi ya wakimbizi wa ndani ya Rimenze ndiyo maskani ya wakimbizi ambao wanatumaini kuwa Sudan itaondoka vitani.

Wakazi wa eneo hilo wanadhani kuna matumaini taifa lao lilipopata uhuru 2011, ungekuwa wakati wa kupumzika na kupunga upepo ili kujenga upya maisha na mustakabali bora.

Lakini, wanakumbuka kuwa miaka miwili baada ya uhuru huo zahma ilizuka upya ikiwamo kwenye kijiji cha Equatorial Magharibi ambako maelfu ya watu walikabiliwa na ukatili mkubwa pamoja na kudhalilishwa kingono na kulazimishwa kufungasha virago .

Mkimbizi Rutto anayeishi humo anasema: “Katika mkasa huo nyumba yangu ilichomwa moto mara mbili, mwaka wa kwanza nilikimbilia katika kambi hii na nikaikarabati utulivu uliporejea, kisha ikateketezwa tena, haya ndio madhila ninayoyapitia.”

Kwa kuwa sasa anaishi kwenye kambi ya wakimbizi na familia yake Rotto hawezi tena kupata kipato kutokana na kilimo na badala yake anategemea utengenezaji wanyavu za kuvulia samaki ili kuishi, na kipato anachopata kwa siku ni takribani dola tatu na nusu.

“Hii ndiyo kazi ninayofanya ili kuweza kuishi kwa sababu haturuhusiwi kwenda nje ya kambi kulima.”

Baada ya kuanzishwa serikali mpya ya umoja wa kitaifa hivi karibuni Rotto na wenziwe wanaitaka amani kwa udi na uvumba.

Watoto wa Rotto pia wamezaliwa vitani na anahofia mustakbali wao wasijekupitia kile alichopitia

“Hakuna amani, watoto wangu wawili wamezaliwa vitani. Sijui jinsi gani serikali itawasaidia kukua bila milio ya risasi. Vita vimeathiri akili zao na wamekuwa kama wendawazimu.”

Japo amekatishwa tamaa mara nyingi na mikataba ya amani inayovunjika safari hii anatumaini kwamba fikra zake si sahihi na kwamba viongozi watawapa watoto wake usalama na mustakabali bora wanaostahili.

### AFADHALI YA JANA

Tangu taifa hilo changa kujinyakulia uhuru limekuwa likigubikwa na vita, machafuko na madhila kwa wananchi ambao maelfu wamelazimika kukimbia kutafuta usalama.

UNHCR inasema kufuatia makubaliano ya amani yaliyotiwa saini 2018 kulikuwa na matumaini kuwa yangekuwa msingi wa amani.

Lakini bado kuna changamoto na amani inaonekana kuwa ni tunda la mbali mtini na si rahisi kulivuna.

Akifafanua kuhusu hilo msemaji wa UNHCR mjini Geneva Uswis Charlie Yaxley aliwahi kusema: “UNHCR inaamini kwamba ni muhimu kwa wawakilishi kutoka jamii za wakimbizi na wakimbizi wa ndani, kushiriki kikamilifu katika mchakato wa amani. Mkataba wowote wenye ushawishi ni lazima ujumuishe mawazo bayana na ya wazi kwa ajili ya upatanisho. Mbinu za kupata haki lazima ziwe wazi na za kuaminika. Wasudan Kusini wengi wametawanyika zaidi ya mara moja, na imani yao katika mchakato huu ni muhimu ili ufanikiwe.”

Anazungumzia vijana kuwa ni lazima wawe kipaumbele kwa vijana kwani machafuko yanayoendelea yameathiri kwa kiasi kikubwa watoto ambao ni takribani theluthi mbili ya wakimbizi wote nchini Sudan Kusni.

Shirika hilo la wakimbizi limesisitiza kuwa ili Sudan Kusini iweze kuwa taifa la amani na mafanikio ni lazima kuwahakikishia vijana wa nchi hiyo wakiwemo wakimbizi fursa ya elimu bora na nyingine za kutimiza ndoto zao.

Zaidi ya raia milioni 2.3 wa Sudan Kusini hivi sasa wanaishi kama wakimbizi katika nchi jirani, huku wengine milioni 1.9 ni wakimbizi wa ndani katika taifa hilo, kwa mujibu wa takwimu za 2018 huenda wakawa wengi zaidi. **UN NEWS**

JUKWAA LA VIONGOZI

THOMAS MOTSOAHAE THABANE

# Alivyochomolewa Ikulu kutinga mahakamani



Waziri Mkuu wa Lesotho akifurahia ndoa yake mwaka 2017. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu wa Lesotho, Tom Thabane, (80), ndiye kiongozi wa kwanza Afrika kulazimika kungoka na kuondoka madarakani ili kufikishwa mahakamani kwa tuhuma za mauaji.

Thabane anayeongoza taifa dogo la kifalme la Lesotho , alitinga kizimbani na mkewe Maesaiah Thabane (42), wakidaiwa kuhusika na mauaji ya Liopelo Thabane, mke wa waziri mkuu huyo, aliyeuawa kwa risasi mwaka 2017.

Thabane na mkewe Maesaiah wako nje kwa dhamana wote wakituhumiwa kuua, wakati mkewe huyu anadaiwa kula njama za kumua Liopelo, katika kipindi hicho ambacho wawili hao Thabene na Liopelo walikuwa kwenye mgogoro wa kitalaka, ambao mahakama kila mara ilimpa mshindi mkewe kabla ya kuuliwa.

Kifo cha mwanamama huyo kilitokea June 14, 2017 siku mbili kabla ya kigogo huyo kula kiapo cha kuongoza Lesotho kwa kipindi cha pili.

**HISTORIA**

Thabane alizaliwa Mei 28, 1939 na kuwa Waziri Mkuu kuanzia Juni 2017 hadi Mei 2020. Ni kiongozi wa chama cha 'All Basotho Convention (ABC)'.

Kadhalika Thabane alikuwa kiongozi kwenye serikali ya Waziri Mkuu Pakalitha Mosisili, kuanzia 1998 hadi 2006 akiwa kwenye chama tawala cha 'Lesotho Congress for Democracy ' (LCD), lakini mwaka 2006 kilijitenga na LCD na kiongozi huyo na kuanzisha All Basotho Convention (ABC). Baada ya miaka mitano ya upinzani alianzisha umoja wa vyama 12 katika uchaguzi wa bunge wa 2012 na kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu.

> Mwaka 2020, haukuwa mzuri kwa Thabane, alikutana na nguvu ya umma ikimtaka ajiuzulu kutokana na madai ya kumua mkewe na alilazimika kutangaza Mei 18 kuwa yuko tayari kung'oka ili kujibu mashtaka.



Tom Thabane akiwa madarakani.

Katika uchaguzi mkuu wa 2015 ABC ilitupwa nje ya uongozi baada ya vyama saba kuungana na kuking'oa chama hicho kwa kura, licha ya muungano huo uliokuwa ukiongozwa na Mosisili kuwa na viti vichache kuliko ABC.

Miezi miwili baadaye Thabane alikimbilia Afrika Kusini kwa madai kuwa maisha yake yamo hatarini, akiondoka na viongozi wengine wawili wa upinzani.

Wote baada ya kuishi uhamishoni kwa miaka miwili Februari 2017, walirejea na kushiriki kwenye kura ya kukosa imani na Waziri Mkuu Mosisili na kufanikisha kumng'oa madarakani.Thabane alishinda uchaguzi uliofanyika na kurejeshwa tena kuwa Waziri Mkuu.

**KUNG'OLEWA**

Mwaka 2020, haukuwa mzuri kwa Thabane, alikutana na nguvu ya umma ikimtaka ajiuzulu kutokana na madai ya kumua mkewe na alilazimika kutangaza Mei 18 kuwa yuko tayari kung'oka ili kujibu mashtaka.

Thabane alishtakiwa tangu 2017, hata hivyo alijitahidi kutumia nguvu na kinga yake kikatiba inayomlinda asishitakiwe lakini aligonga mwamba na kutakiwa kujiuzulu na wadau wake wa muungano wa kisiasa na nafasi yake kuchukuliwa rasmi Mei, 2020 na Moeketsi Majoro ambaye sasa ndiye Waziri Mkuu.

**KUTINGA MAHAKAMANI**

Thabane amekuwa kiongozi wa kwanza Afrikan kufikishwa kortini kujibu mashtaka akiwa madarakani. Februari 24 alifikishwa katika mahakama kuu ya Maseru akiwa na mkewe wa sasa wakitakiwa kujibu mashataka ya mauaji hayo. Wote walikana mashtaka na wako nje kwa dhamana.

Lipolelo Thabane (58) aliuawa kwa kupigwa risasi za karibu mara kadhaa akiwa kwenye gari lake karibu na nyumba yake siku kabla ya mumewe kula kiapo mkasa uliotokea 2017.

Mkewe huyo alikataa kupewa talaka na Thabane na kushika kesi mahakama iliyompa haki ya kuendelea kuwa Mke wa Waziri (first lady) na kupatiwa stahiki zote kama mke wa kiongozi wa serikali na taifa hadi watakapotengana rasmi na mumewe.

Kiongozi huyo baada ya miezi mwili ya kumzika mkewe, alioa na kwa pamoja wamefikishwa mahakamani kujibu mashtaka ya mauaji licha ya msemaji wake kusema kuwa alikuwa analindwa na ana kinga ya kikatiba japo hakuwa juu ya sheria.

Kiongozi huyo alikataa kuondoka Ikulu akieleza nia yake ya kujiuzulu Julai, hata hivyo washirika wake walimtimua wakimtaka kuondoka mapema na haraka zaidi shinikizo likitoka chama cha All Basotho Convention.

Wahusika wa mauaji hayo wanadaiwa kuwa walikodiwa kutoka Afrika Kusini na kwa kipindi kirefu tangu Maesaiah, alipoingia madarakani amekuwa akituhumiwa kuwaondoa yake na Waziri Mkuu ilikuwa inaingilia taratibu za kisiasa. Aidha, anadaiwa kujipatia kiufisadi na kwa njia ya kutakatisha fedha, pesa alizoitumia kuanzisha mfuko wa kusaidia wananchi kuondoa umaskini.

Januari mwaka huu Waziri wa Fedha wa Afrika Kusini Tito Mboweni, alipendekeza Lesotho iwe sehemu ya Afrika ya Kusini chini uamuzi utakayofanywa kwa utaratibu wa kuunda shirikisho, kauli aliyoitoa Februari 26, 2020.

**MKEWE KUTWAA UONGOZI?**

Mei mwaka 2018, taasisi ya mkewe Thabane ya Maesiah Thabane Trust Fund, ilidai mkurugenzi wake Makarabo Mojakhomo na mumewe aliyekuwa ofisa wa Wizara ya Mambo ya Ndani Thabang Mojakhomo, walihujumu taasisi hiyo kwa kuiibia mamilioni ya fedha.

Baadaye zilitolewa taarifa za Makarabo kutoweka akiwa rumande na Shirika la Kimataifa la Kutetea Haki za Binadamu (AI),liliandika tangazo la hofu ya familia ya Makarabo kuwa ametoweka kitatanishi na kwamba nchi hiyo ina historia ya watu kutoweka 'kienyeji' unaohusisha nguvu za dola.

Baadaye Mojakhomo alionekana Afrika Kusini na kueleza kuwa ana wasiwasi kwa kuwa 'Fisrt Lady' au mke wa Waziri Mkuu Maesiah ana nguvu za kudhibiti polisi na kuingilia mwenendo mzima wa mahakama na kulalamika kuwa hatatendewa haki.

'Mama Thabane' alituhumiwa na Motlohi Maliehe, Waziri wa Utalii na mazingira na utamaduni ambaye pia ni mwenyekiti wa chama cha ABC kuwa ni mbadhirifu.

Waziri huyo alifukuzwa kazi baada ya madai kuwa Thabane, alikuwa anaingilia na kuvuruga serikali akitaka kuingilia uongozi na serikali na kuwabana mawaziri wamsikilize na kutekeleza yale anayowaagiza kwenye kufanya majukumu yao. **MITANDAO**



## Hospitali ya rufani yaagizwa kuboresha huduma kwa wananchi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MGANGA Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, ameuagiza uongozi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kuboresha huduma za tiba kwa wananchi wanaofika kupata huduma za afya katika hospitali hiyo.

Prof. Makubi alitoa maagizo hayo jana baada ya kufanya ziara ya kushtukiza kwenye hospitali hiyo na kushuhudia kero mbalimbali ikiwamo baadhi ya wagonjwa kuchelewa kupewa huduma, madaktari bingwa kutowaona wagonjwa kwa wakati na huduma za vipimo kuchelewa.

Alisema ni vyema uongozi wa hospitali hiyo kushughulikia kero hizo ili wananchi wapate huduma bora.

"Yapo mazuri tumeona mnayofanya kwa wananchi na tunawapongeza, ila lazima kuangalia upande wa pili ambao wananchi wanayataka, kwa yale mapungufu tuliyoyaona tungependa kuona yanaboreshwa haraka ili hospitali hii iwe ya mfano kwa hospitali zote za rufani za mikoa kwa kutoa huduma zilizo bora," alisema.

Prof. Makubi alisema hospitali hiyo inatakiwa kuonyesha mfano kuanzia utoaji wa huduma bora kwa mteja pamoja kupunguza muda wa wagonjwa kusubiri huduma, upatikanaji wa wauguzi na mabingwa wanapohitajika na usafi wa wodi kwani ndiyo chachu ya wananchi wengi kufika hapo na kupata huduma kabla hawajapewa rufaa ya kwenda hospitali kubwa kama Benjamin Mkapa.

Aidha, aliutaka uongozi na watumishi wa hospitali hiyo kutambua majukumu yao kwa kuonesha kuwajali wananchi wote na kuwataka kuweka utaratibu usio na usumbufu kwa wagonjwa na kupatiwa huduma kwa wakati.

Prof. Makubi alionyesha kusikitishwa alipokuta wodini baadhi ya wagonjwa wamelazwa na hawajaonwa na mabingwa kwa zaidi ya siku tatu, wauguzi wakiwa hawajaambatana na madaktari katika kuzungukia wagonjwa huku madaktari wa vitendo wakifanya peke yao bila uangalizi.

"Baadhi ya wagonjwa wengine wamelazwa chini wakati vitanda viko wazi pamoja na mazingira ya wodi kutoridhisha na kukosekana kwa mpangilio wa vifaa, lazima watumishi mjitambue mko wapi kwani awamu hii ni ya kuwajali wanyonge na kufanya kazi kwa bidii ndio kanuni ya awamu hii hapa kazi tu," alisisitiza.

Aliwataka madaktari wa hospitali hiyo kufanya kazi kwa ushirikiano na wauguzi katika kuwahudumia wagonjwa.

# Lukuvi aagiza kukamata watakaouza ardhi Mtakuja

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameagiza kukamatwa mtu yeyote atakayethubutu kuuza ardhi katika Mtaa wa Mtakuja, Kata ya Chang'ombe jijini hapa hadi hapo utakapomalizika mgogoro uliopo.

Eneo hilo linadaiwa kuwa na mgogoro uliodumu kwa miaka 44 licha ya viongozi mbalimbali kwenda na kuunda kamati ya kutatua lakini ufumbuzi bado haujapatikana.

Akizungumza na wananchi wa eneo hilo, Waziri Lukuvi alisema amepokea taarifa kutoka kwa kamati iliyoundwa awali, lakini ameona bado kuna mapungufu mengi na hivyo kutoa miezi mitatu kwa kamati kufanya uhakiki tena.

"Naomba mvumilie hakuna kuongeza choo, kujenga wala kupasua barabara wala kufanya nini mpaka taarifa ya mwisho itakapotolewa tunataka taarifa tutakayoisoma leo hadi siku tunakuja iwe hiyo hiyo, kama una haki yako upewe haki yako kwa mali tuliyoikuta leo," alisema.

Aliwaonya watu wanaojenga usiku na baadhi ya watu wanauza uza ardhi kwenye eneo hilo, huku akiagiza wakamatwe watakaobainika kufanya hivyo.

"Kuna watu wanajifanya vidume kuuza uza hapa kamateni, ardhi ibaki hivi hivi, taarifa hizi ziwakute kama mlivyo na baada ya hapo nitaletewa," alisema.

Alisema serikali itahakikisha kila mwenye haki anapata.

"Miezi mitatu sio mingi baada ya hiyo taarifa itakuja kwangu moja kwa moja na ikiwa mwezi wa Oktoba au Novemba vyovyote vile nitaomba kibali kwa Mkuu wa Mkoa nitakuja, mimi nimetumwa kufanya kazi hii hatutashindwa nitahakikisha tunalinda kila haki ya mtu," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa huo, Hemed Seleman, alisema kutokana na mgogoro huo amekuwa akipata wakati mgumu kutokana na wananchi kutoa malalamiko mara kwa mara kuhusu ardhi hiyo na kumwomba waziri huyo kuwatatulia.

"Nimefarijika na ujio wa Waziri Lukuvi na kwa maamuzi aliyoyatoa naunga mkono asilimia 100, nyumbani kwangu kulikuwa kama hospitali kila mtu anakuja na matatizo yake, kweli kuna watu wanauza viwanja wakati mwingine hadi usiku nashirikiana na wananchi kuwatimua watu hao, naomba waziri akija tena aje kutatua tatizo hili," alisema.

Nao baadhi ya wananchi walisema kutokana na mgogoro huo wameshindwa kupata maendeleo kwa muda mrefu ikiwamo kujengewa miundombinu.



Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna (kulia), akizungumza na viongozi na wafanyabiashara wa soko la Sabasaba, jijini humo juzi, akiwataka kutoa ushirikiano kwa halmashauri ya jiji hilo, na kuacha kuvamia maeneo yasiyo rasmi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mbaroni madai kukutwa na shehena ya dawa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

JESHI la Polisi mkoani Dodoma limewakamata watu wawili baada ya kukutwa na shehena ya dawa za hospitali za aina mbalimbali.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Gilles Muroto, alisema alisema dawa hizo zina nembo ya Bohari ya Dawa(MSD) na zimewasili Dodoma kwa ajili ya kuuza katika maduka binafsi ya dawa.

"Julai 9, mwaka huu alikamatwa Fredrick

Anaclet Maxmillian (38) ambaye ni mkazi wa Mbagala jijini Dar es Salaam, akiwa na shehena ya dawa mbalimbali sampuli 149 na katika mahojiano ya awali mtuhumiwa huyo sio mfamasia wala si daktari anashirikiana na mfamasia ambaye ni mtumishi wa serikali jina limehifadhiwa huko mkoani Tabora," alisema.

Kamanda huyo alisema uchunguzi bado unaendelea na wote waliohusika kushirikiana na mtuhumiwa huyo watatafutwa na kufikishwa mahakamani.

Katika hatua nyingine, Muroto alisema vikao vya Chama Cha Mapinduzi(CCM) vilivyofanyika kuanzia Julai 9 hadi 12, mwaka huu vimeisha salama huku akimpongeza Rais John Magufuli kwa kuendesha kwa muda mfupi ikilinganishwa na hapo awali vilikuwa vikiisha usiku wa manane.

"Nampongeza pia Mkuu wa Polisi (IGP), Simon Sirro, kutokana na kuniamini katika utendaji kazi, kwa kuwa kipindi hicho chote hakuna mjumbe au mgeni au mtu yeyote aliyepata madhara ya kiuhalifu," alisema.

Muroto pia alimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kuviongoza vyombo vyake vizuri ambavyo vimefanya kazi yake kwa ufanisi mkubwa na kuifanya Dodoma kuwa salama wakati wowote.

"Bila kuwasahau wananchi wa Dodoma wakiwamo wafanyabiashara kwa huduma za kijamii na ukarimu walioonyesha kwa wageni wa mkutano mkuu," alisema.



## Wito wajumbe TSC kusimamia misingi, nidhamu ya taaluma

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Kivuma Msangi, amewakumbusha wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuendelea kusimamia misingi na nidhamu ya taaluma.

Amewakumbusha wajumbe hao kuwa wahakikishe wanazingatia sheria ili waweze kutenda haki.

Msangi alitoa kauli hiyo wakati wa shughuli za kuwaapisha wajumbe wapya waliochaguliwa na TSC ambao walichaguliwa kwa ajili ya kusimamia masuala ya nidhamu, rufani ngazi ya wilaya pamoja na maendeleo kwa walimu wa shule za msingi na sekondari.

Msangi aliwataka wajumbe wa TSC ngazi ya wilaya kushughulikia masuala ya kinidhamu ya walimu kwa kufuata sheria zilizopo, ili waweze kutenda haki kulingana na makosa yaliyofanywa.

Aliwataka wateule hao kuwa waadilifu na makini katika kufanya uchunguzi pamoja na maamuzi kwa kufuata miongozo, waraka na sheria bila ya kumwonea yeyote au kusikiliza shinikizo la mtu, huku akisisitiza kwa wakuu wa shule za sekondari na msingi kufanya ufuatiliaji wa walimu ili kuondoa migogoro ambayo itaathiri na ufaulu kwa wanafunzi.

"Mwaka 2019 Wilaya ya Mbarali ilipata usajili wa shule mbili za sekondari na mwaka huu wamepata usajili wa shule sita za sekondari pamoja na za kidato cha tano na sita mbili, lakini usajili wa shule nne za msingi na wanatarajia kupata usajili wa shule za sekondari tatu ifikapo mwaka 2021," alisema na kuongeza:

"Haya yote yanaashiria kuwa kuna umoja na mshikamano kati yenu naipongeza tume iliyopita pamoja na walimu wote kwa hatua hii."

Mwenyekiti wa Kamati Mpya ya TSC, Mwalimu Stella Mbinda, aliahidi kufanya kazi kwa kuzingatia weledi, maadili na umakini mkubwa bila ya kumwonea yeyote, huku akiomba ushirikiano katika kutekeleza masuala hayo.

Katibu wa Tume hiyo, Mwalimu Issa Shemgei, alisema kuwa kwa mwaka 2016 hadi 2020 walipokea masuala ya kinidhamu 37 kati ya mashauri hayo walimu 24 walifukuzwa kazi, saba walipewa karipio, mmoja onyo, mmoja alishushwa cheo na wengine wanne wanasubiri uchunguzi na maamuzi ya kamati.

Shemgei aliongeza kuwa katika kipindi hicho jumla ya walimu 99 waliajiriwa huku walimu 377 wakipandishwa vyeo na walimu 76 wakibadilishwa vyeo kimuundo baada ya kujiendeleza kielimu kwa ngazi mbalimbali.

# Aina tatu za mbegu ulezi zabuniwa

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole imebuni aina tatu za mbegu za ulezi ambazo ni U- 15, Tari FM1 na P 224 zitakazoanza kusambazwa kwa wakulima wa maeneo kadhaa nchini.

Hatua hiyo ni moja ya mikakati ya kulifufua zao hilo ambalo linasuasua hivi sasa.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, wakati wa kukagua na kuangalia maendeleo ya kilimo cha ulezi eneo la kituo hicho.

Dk. Bucheyeki alisema zao la ulezi lina manufaa kwa afya ya watumiaji kwa sababu lina madini mengi ambayo yanaimarisha na kumfanya mtu awe imara na asizeeke mapema.

Alisema zao hilo linapandwa mikoa yote nchini na kwamba mbegu hizo zina uwezo wa kutoa magunia kuanzia 13 hadi 40 kwa ekari moja wakati mbegu za zamani zilikuwa zinatoa magunia sita tu, na kwamba mkulima anaweza kupata kiasi cha fedha Sh. milioni 32.

Alifafanua kuwa watatumia mbinu mbalimbali kusambaza mbegu hizo ili ziwafikie wakulima kirahisi ikiwamo matumizi ya mitandao ya kijamii na vipeperushi na vyombo vya habari.

"TARI Uyole tumekuja na mbinu ya haraka ya kusambaza teknolojia kwa wakulima wetu... tunaamini kuwa na mbegu hizo zinaweza kupandwa mikoa yote ya Tanzania na mwakani tutambulisha mbegu nyingine yenye madini ya zinki ambayo inaongeza nguvu ya kiume," alisema Dk. Bucheyeki.

Mtafiti Mwandamizi wa zao la ulezi kutoka TARI Kituo cha Uyole, Dk. Denis Tippe, alisema kazi yao kubwa kwa sasa ni kulifufua zao hilo ambalo mwitikio wa kulima ni mdogo kulinganisha na ilivyokuwa awali.

Alisema wanalifufua zao hilo ili kuimarisha afya za wananchi na kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja kwa kuhakikisha linakuwa ni miongoni mwa mazao yanayopewa vipaumbele.

Dk. Tippe alisema licha ya kituo hicho kuzalisha mbegu hizo za ulezi, wamewakasimisha madaraja ya uzalishaji kwa baadhi ya wakulima wakiwamo wa Singida, Mbozi, Sumbawanga na Nkasi.

"Kazi yetu kubwa sasa ni kuwaambia wakulima kuwa zao hili sasa lilimwe kama mahindi au maharage kwa sababu kilimo chake hakihitaji tena kufyeka pori muhimu ni mbolea na kuzingatia upandaji wa sentimita 50 kwa 50 kutoka kila mbegu," alisema na kuongeza:

"Mavuno yake ni magunia 40 kwa ekari moja na wakulima watakuwa wamevuka wastani wa Taifa wa tani moja kwa hekta moja na kufikia tani mbili."

Aliongeza kuwa zao la ulezi halishambuliwi na magonjwa na linahimili mazingira yoyote ya hali ya hewa na linahifadhika vizuri ambapo linaweza kukaa kwa muda mrefu baada ya kuvunwa wa wastani wa zaidi ya miaka mitano.

Ofisa Usambazaji wa Teknolojia Kituo cha Uyole, Rehema Ole-Seenga, hivyo aliwataka wamebuni teknolojia zinazohusu mazao mbalimbali nchini, ambapo aliwakumbusha wakulima kuzingatia maelekezo ya wataalamu ili kuongeza uzalishaji na kupata faida.



Mtafiti mwandamizi wa zao la ulezi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole, Dk. Denis Tippe (kushoto), akionyesha moja ya aina ya mbegu inavyostawi katika eneo la shamba la kituo hicho, jijini Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Bil. 18/- kumaliza kero ya maji Rungwe

**Na Grace Mwakalinga, RUNGWE**

ZAIDI ya Sh. bilioni 18 zimetolewa na serikali ili kukamilisha miradi mbalimbali ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji kwa uhakika.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, wakati wa kikao kilichohusisha jumuiya ya watumia maji ambacho kiliwahusisha wataalamu na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA).

Alisema kwa sasa wilaya hiyo inapata huduma ya maji kwa asilimia 73 na kwamba baada ya miradi yote inayotekelezwa kukamilika watakuwa wamefikia lengo la serikali la upatikanaji wa maji kwa asilimia 85 kwenye maeneo ya vijijini.


"Fedha hizo zimeelekezwa kwenye maeneo mbalimbali ya kujenga miradi ya maji ikiwamo eneo la Mwakaleli kiasi cha shilingi bilioni sita, Masoko shilingi bilioni tano na maeneo mengine kama Isyonje na Ikuti wanaendelea na miradi na baada ya kukamilika, tatizo la maji kwa wananchi litakuwa la kihistoria," alisema Chalya.

Aliongeza kuwa licha ya jitihada za serikali katika kutatua tatizo la maji kwa kuanzisha miradi, lakini kulikuwa na ubadhirifu hususani kwa jumuiya za watumiaji wa maji, hivyo miradi mingi kushindwa kufikia malengo.

Kutokana na vikwazo hivyo, Chalya alizitaka mamlaka zote zinazohusika na utoaji huduma za maji hususani RUWASA kuhakikisha zinaisimamia vyema jumuiya za watumia maji ili kuondoa uchakachuaji wa fedha kwenye miradi.

Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini Mkoa wa Mbeya, Mathayo Athuman, alisema chombo chochote cha kusimamia maji kwa mujibu wa sheria za maji inabidi kujisajili upya ili kuendesha shughuli zake.

Alisema utaratibu wa vyombo vya maji kujisajili upya kabla ya kuendelea na shughuli kama lilivyotakwa la kisheria umefikia asilimia 74 kwa Mkoa wa Mbeya.





# ZAECA kuelimisha wananchi kukataa rushwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), imesema itaendelea kutoa elimu kwa wananchi, taasisi za serikali na binafsi ili kuepusha rushwa hasa katika kipindi hiki cha kueleka uchaguzi mkuu.

Hayo yalielezwa na Kaimu Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma kutoka ZAECA, Sheha Kombo Hamad, wakati wa majumuisho ya utoaji wa elimu ya kukabiliana na maafa kwa majimbo ya Mkoa wa Magharibi Unguja kichama.

Alisema Chama Cha Mapinduzi kimeweka utaratibu maalum wa kuwapata viongozi wake hivyo hakitoweza kuwafumbia macho watakaobainika kupokea au kuchukua rushwa.

Alisema serikali imeweka mikakati na mipango mbalimbali ya kukabiliana na suala hilo kwa kuwa ni adui wa haki na inarudisha nyuma maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Katibu wa CCM Mkoa wa Magharibi, Mgeni Mussa Haji, alisema wameandaa mafunzo kwa kamati za siasa katika majimbo, wadi na matawi katika mkoa huo ili wazidi kupata uelewa wa kujikinga na utumiaji wa rushwa katika maeneo yao.

Aliiomba ZAECA kufuatilia mwenendo wa rushwa kwa vyama vingine badala ya kuegemea CCM pekee kwa kuwa na vyenyewe ni sehemu ya jamii.

**Katibu wa CCM Mkoa wa Magharibi, Mgeni Mussa Haji, alisema wameandaa mafunzo kwa kamati za siasa katika majimbo, wadi na matawi katika mkoa huo ili wazidi kupata uelewa wa kujikinga na utumiaji wa rushwa katika maeneo yao.**

# Hamad Rashid aahidi kudumisha Muungano

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MWENYEKITI wa Chama cha ADC Taifa, Hamad Rashid Mohammed, amesema kama atapata ridhaa ya kuongoza Zanzibar, ataendelea kudumisha Muungano wa Zanzibar na Tanganyika kwa sababu ndio uliowakomboa wananchi.

Aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wanachama wa chama hicho waliofika kumdhamini baada ya kuchukua fomu ya kuwania urais.

Alisema chama chake kitaendelea kuheshimu mfumo uliopo wa Serikali ya Zanzibar hadi hapo wananchi watakapofikiria kufanya uamuzi mwingine.

Alisema wapo baadhi ya wanasiasa wanaoubeza wakati idadi kubwa ya Watanzania wamezaliwa ndani ya Muungano.

"Chama chetu kitaendelea kusimamia Muungano na mfumo wa sasa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar," alisema.

Alisema chama hicho kinaamini kero zilizopo za Muungano suluhu yake ni kuendelea kukaa pamoja kuzungumza.

Hamad alisema anagombea nafasi hiyo ili kuendeleza mazuri yanayoachwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein.

Aliwaomba wanachama kuendelea kudumisha amani na kuviheshimu vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuwa vinafanya kazi ya kusimamia amani.

Alikipongeza chama kwa kumpa nafasi ya kuwa Mwenyekiti wa Taifa na kwa mujibu wa Katiba Mwenyekiti anaweza kukaa madarakani kwa vipindi viwili vya miaka mitano.

Naye Mkurugenzi wa Uchaguzi wa chama hicho, Omar Albet Costine, alisema hawana shaka na mgombea wao kwa kuwa amefanya kazi nzuri katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo anaendelea kuhudumu kama Waziri wa Afya.



Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Zanzibar, Dk. Mzuri Issa (katikati), akiangalia bidhaa za wajasiriamali kutoka Pemba, waliozipeleka katika ofisi za chama hicho, Tunguu juzi, kwa ajili ya kutafutiwa masoko. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wazazi wahamasishwa kuchanja watoto

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZAZI na walezi wametakiwa kuwapeleka watoto wao kliniki kupata chanjo ili kuwakinga na maradhi.

Mratibu wa kitengo cha chanjo Zanzibar, Dk. Abdulhamid Ameir Saleh, alitoa wito huo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mafunzo ya siku moja kuhusu chanjo.

Alisema katika kipindi hiki cha ugonjwa wa Covid-19, mwamko wa wanawake kuwapeleka watoto wao kliniki ni mdogo.

Ofisa Mdhamini Wizara ya Afya Pemba, Shadya Shaaban Seif, aliwaomba wazazi kuwapeleka watoto wanaostahili chanjo katika vituo vya afya ili kuwakinga na maradhi.

Alisema imethibitika kuwa chanjo ni mkakati muafaka katika kutokomeza maradhi na kupunguza vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Licha ya changamoto hizo, alisema Zanzibar imefanikiwa katika utoaji chanjo kwa watoto hali ambayo imesaidia kupunguza maradhi.

Ofisa Uendeshaji wa kinga kutoka Wizara ya Afya Pemba, Dk. Yakub Mohamed Shoka, alisema chanjo ni suala la ulimwengu, hivyo kila mtoto anapaswa kupatiwa kwa wakati.

Kwa upande wake, ofisa kutoka kitengo cha chanjo Pemba, Bakar Hamad Bakar, alisema malengo ya mkutano huo ni kupata taarifa ya mwenendo wa chanjo na saratani ya shingo ya mlango wa kizazi kwa wasichana wenye umri wa miaka 14.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


### KUPOTEA KWA CHETI



**PHILIP MAGHOLA MALACH** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0533-055 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia SARWATT mwaka 1991. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: DAR/KIJ/RB/528727/2020.**

158117

### KUPOTEA KWA CHETI



**BONIFACE AZARIA MBUYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0356/0077** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia VUNJO SEKONDARI mwaka 1988. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHU/RB/481374/2020.**

115811102

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GODWIN ANDREW KIRENGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 938 DLA SUZUKI.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: DAR/MBU/R-B/524261/2020.**

158117

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 75/2020**

Ombi la **MARY MWAIPOPO** kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **CHRISTINA MWAIPOPO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 24/07/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 13/07/2020.

Sahihi ya Hakimu

158118

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO MJINI**
**WILAYA YA DODOMA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**SHAURI LA MADAI 289, 290 na 291 YA 2020**
**MDAI.......................... WANTORA JN BUSINESS SOLUTION CO. LTD**
**DHIDI YA**
**WADAIWA...................**
**1. ELIPIDIUS GERVAS BENEDICTO**
**2. SCARIUS KAIZA 3. IDRISA ISSA ALLY.**

Kwa kuwa mdai mtajwa hapo juu alifungua mashauri dhidi yenu wadaiwa watajwa hapo juu. Mnaamriwa na Jamhuri kuhudhuria mbele ya Mahakama hii mnamo tarehe 21/07/2020 bila kukosa ili kujibu madai hayo dhidi yenu. Endapo hamtahudhuria mbele ya Mahakama siku hiyo shauri/mashauri hayo yatasikilizwa upande mmoja (Exparte Hearing) na kutolewa maamuzi.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na Mahakama hii leo tarehe 14/07/2020.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO MJINI
DODOMA

151816

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;183/2020**

Ombi la EVELINA G.DIMINOFF,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ONESMO BENEDICTO KAHATANO. Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 23/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/07/2020.

Sahihi ya Hakimu

158122


***Kwa Habari Motomoto***

***usikose Gazeti lako la***

***Nipashe kila siku***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HABARI PICHA



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa Arusha, Mrisho Gambo, akikabidhiwa fomu ya kuwania kugombea nafasi ya Ubunge Jimbo la Arusha mjini, kutoka kwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Arusha, Denis Mwita, jijini humo jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**



Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (katikati), akikabidhiwa fomu ya kuwania nafasi ya ubunge Jimbo la Mbeya Mjini kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Katibu wa chama hicho, Mbeya Mjini, Gervas Ndaki, katika ofisi za CCM Wilaya ya Mbeya jana. Kulia ni mume wake, James Andilile Mwainyekule. **PICHA: BUNGE**



Katibu wa Umoja wa Vijana wa CCM, Wilaya ya Kigoma Mjini, Emmanuel Shitobelo (kulia), akimkabidhi fomu ya kuomba ridhaa ya kugombea ubunge katika Jimbo la Kigoma Mjini, Dk. Juma Mwaka Juma, eneo Ujiji Manispaa ya Kigoma/Ujiji jana. **PICHA: JOCTAN NGELLY**



Katibu wa UVCCM, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, Ally Simba (kulia), akimkabidhi fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea ubunge katika Jimbo la Kawe, kwa kada wa chama hicho, Mulla Nawah. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Katibu wa CCM Wilaya ya Ilala, Iddi Mkowa (kushoto), akimkabidhi fomu ya kuwania kuteuliwa kugombea ubunge Jimbo la Segerea, Joyce Maduro, kada wa chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Watia nia wa nafasi ya ubunge katika majimbo matatu ya Kahama Mjini, Ushetu na Msalala, wakiwa wamekaa mstari wa kuingia ofisini kwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga jana, kwa ajili ya kuchukua fomu ya kuomba ridhaa ya kugombea nafasi hiyo. **PICHA: SHABAN NJIA**



# SANE APAGAWA MAZOEZI BAYERN




**MUNICH,** Ujerumani

LEROY Sane amesema "alikuwa na furaha isiyo kifani" kuwa Bayern Munich baada ya kuanza mazoezi yake ya kwanza tangu ajiunge na klabu hiyo.

Bayern waliweka picha kwenye kurasa zao za mitandao ya kijamii zikimwonyesha Sane akiwa kwenye mazoezi Jumatatu, huku winga huyo akiwa pamoja na mchezaji mwenzake mpya, Niklas Sule.

Raia huyo wa Ujerumani alijiunga na miamba hao wa Bundesliga kutoka Manchester City katika dili lililogharimu kiasi cha euro milioni 60 mwezi huu, akisaini mkataba wa miaka mitano kukaa na klabu hiyo ya ardhi ya nyumbani kwao.

"Ilikuwa nzuri sana," Sane alisema kupitia video iliyowekwa kwenye mitandao ya kijamii.

"Lilikuwa ni kundi dogo na nilifanya mazoezi na Niklas Sule, lakini ilikuwa poa sana kuwa uwanjani tena, kumaliza kipindi changu cha kwanza cha mazoezi.

"Nina furaha isiyo kifani hapa."

Sane ilionekana angehamia Bayern mwaka jana, lakini aliumia goti wakati wa mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Liverpool.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, aliichezea City dakika 11 tu kwenye Ligi Kuu msimu huu, huku Pep Guardiola akibainisha kwamba klabu hiyo ilishindwa kumshawishi mchezaji huyo kusaini mkataba mpya.

Bayern imeshathibitisha kwamba, Sane atavaa jezi namba 10 msimu ujao, ambayo ilikuwa ikivaliwa na Philippe Coutinho wakati akicheza hapo kwa mkopo wa muda mrefu akitokea Barcelona.

# Zidane akataa, agoma ubingwa

**MADRID,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Zinedine Zidane amesisitiza ubingwa wa LaLiga bado uko mbali baada ya vinara hao kujisogeza karibu zaidi na taji hilo.

Madrid sasa inahitaji kushinda mchezo mmoja tu ili iweze kuwapiku Barcelona kulitwaa taji hilo, baada ya kupata ushindi wa 2-1 Jumatatu dhidi ya Granada.

Ferland Mendy alifunga bao la kwanza kwa Madrid na Karim Benzema akafunga la pili kuwawezesha Los Blancos kuongoza msimamo kwa tofauti ya pointi nne dhidi ya Barca, huku zikiwa zimesaliwa mechi mbili msimu kumalizika.

Madrid wanaweza kulitwaa taji hilo kwa mara ya pili kati ya misimu nane kama watashinda mchezo wa nyumbani dhidi ya Villarreal Alhamisi, lakini Zidane aliepuka kuzungumzia kulikaribia taji hilo.

"Tulikuwa na kipindi kizuri sana cha kwanza, tukicheza kwa kujituma na kumiliki mpira," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari.

"Kipindi cha pili hakikuwa kizuri, lakini ni kwa sababu wapinzani wetu walicheza vizuri zaidi.

"Kupata kitu fulani kwenye LaLiga, unatakiwa kujituma na kwa msimu wote na hivyo ndivyo timu imekuwa ikifanya.

"Tunatakiwa kujivunia timu. Tuna mechi mbili zimebaki na hatujashinda chochote bado."



# Conte: Nipo tayari kuondoka Inter



**MILAN,** Italia

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte amesema "hatasita" kuondoka kama klabu haitakuwa na furaha naye, ingawa Muitaliano huyo bado ana majukumu na Nerazzurri hao licha ya majaliwa yake kuwa shakani.

Conte alijiunga na Inter mwanzoni mwa msimu huu, lakini kumekuwa na ripoti kwamba, kocha huyo wa zamani wa Chelsea na Juventus anaweza kuondoka mwishoni mwa msimu huu wa 2019-20.

Mashaka yameibuka baada ya Inter kutokuwa kwenye kiwango chake na jambo linalomchanganya Conte, wakishindwa kuonyesha kiwango chao tangu kurudi kwa Serie A mwezi uliopita baada ya msimu kusimama Machi mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Inter waliwapiku Lazio na kujivuta nafasi ya pili kwenye msimamo nyuma ya vinara Juve, huku zikiwa zimesalia mechi sita ligi kumalizika, baada ya Jumatatu kushinda 3-1 dhidi ya Torino nyumbani na Conte aliulizwa kuhusu majaliwa yake.

"Niliitwa Inter kwa mradi wa miaka mitatu, kuwarudisha pale walipokuwa wanastahili," alisema Conte akiiambia Sky Sport Italia.

"Kwa uhalisia hilo linachukua muda. Nilikuja hapa na matarajio makubwa. Nina imani.

"Nilianza mradi wa miaka mitatu na (mkataba wangu) unamalizika baada ya miaka mitatu. Baada ya hapo, kama wanataka kuongeza mkataba wangu... nitafurahi, najua kuna safari ndefu ya kwenda, lakini sitaki kupitiliza muda wa kukaa hapa.

"Kama kila mtu ana furaha kwa kazi ninavyofanya, na nafikiri hilo ndio jambo lililopo kwa sasa, kutoka kile nilichoombiwa, hivyo sioni kwa nini tutatakiwa kuendelea kuwa pamoja."

# Pellegrini na mkakati kuipeleka Betis Uefa

**MADRID,** Hispania

MANUEL Pellegrini ana matumaini kuiwezesha Real Betis kutoa changamoto ya kupambana kupata nafasi ya kufuzu kucheza mashindano ya Ulaya msimu ujao.

Betis wiki iliyopita ilimtangaza Pellegrini kama kocha wake mpya kwa mkataba wa miaka mitatu, ingawa mkurugenzi wa michezo, Alexis Trujillo atakuwa kocha wa muda hadi mwishoni mwa msimu huu.

Trujillo aliteuliwa kuwa kocha wa muda baada ya kufukuzwa kwa Rubi ikiwa ni baada ya mechi tatu tu tangu kurudi tena kwa LaLiga iliposimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Betis wapo nafasi ya 13 kwenye LaLiga lakini Pellegrini, ambaye aliipeleka Villarreal kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2006 na Malaga kwenye robo fainali ya mashindano hayo mwaka 2013, ana matumaini ya kupata tena mafanikio.

Klabu hiyo ilifikia hatua ya 32 kwenye Ligi ya Europa msimu uliopita, ikiwa ni mara ya kwanza kucheza katika mashindano hayo tangu walipotolewa kwa mikwaju ya penalti na Sevilla mwaka 2014, na walishiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya



# BARCELONA WAENDELEA KUKOMAA NA MARTINEZ




**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA bado inawania kumsajili nyota wa Inter Milan, Lautaro Martinez mwishoni mwa msimu huu, kwa mujibu wa ukurasa wa kwanza wa gazeti la Mundo Deportivo la jana Jumanne.

Kwa miaka kadhaa Lautaro amekuwa akitajwa kuwa anaondoka Inter kwenda Barcelona.

Barca wanamwangalia nyota huyo wa kimataifa wa Argentina kama mrithi wa muda mrefu wa Luis Suarez, ingawa mlipuko wa virusi vya corona unaonekana kuwa na athari kwenye mipango yao ya usajili.

Hata hivyo, bado Barcelona imeonyesha nia ya kutaka kumsajili nyota huyo ili kuimarisha kikosi chao.

Mpango huo wa Barca kwa Martinez unaweza usifanikiwe kutokana na kiwango cha fedha kinachotakiwa kwa ajili ya usajili wake, ambapo mkataba wake unasema auzwe kwa euro milioni 111. Hata hivyo, kocha wa Barca, Quique Setien ameripotiwa kufikiria mpango mwingine wa kuwauza nyota watatu ili kuweza kumpata Martinez.

Ousmane Dembele anaweza kuuzwa kwa ajili ya kupata fedha pamoja na Arturo Vidal, Ivan Rakitic na Samuel Umtiti wanaweza kupendekezwa wachukuliwa Inter ili kukamilisha dili hilo.

# *Lampard: Sikutegemea mbeleko ya Manchester City*

**LONDON,** England

FRANK Lampard amesisitiza kamwe Chelsea haikuwa inategemea 'mbeleko' ya kufungiwa kwa Manchester City kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kutawapa wao nafasi ya kufuzu.

City walifungiwa miaka miwili kushiriki mashindano ya Ulaya na kupigwa faini ya euro milioni 30 kwa kukiuka kanuni ya usawa kwenye matumizi ya fedha katika usajili wa wachezaji na Shirikisho la Soka Ulaya (Uefa), Februari mwaka huu.

Lakini mahakama ya usuluhishi wa michezo, CAS, iliifuta adhabu hiyo Jumatatu baada ya City kukata rufani, hiyo ikiwa na maana kwamba mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England msimu wa 2018-19 watashiriki mashindano ya Uefa msimu ujao, huku faini ikishushwa hadi euro milioni 10.

Maamuzi hayo ya CAS maana yake sasa ni kwamba timu nne tu za juu kwenye Ligi Kuu England ndizo zitakazofuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya na City tayari imejiimarisha kwenye nafasi ya pili.

Pointi sita zimezitenganisha timu tano katika mbio za kuwania kumaliza nafasi ya nne na Lampard amebaki ametulia na hana wasiwasi kwa hilo.

"Kwa uhakika kabisa sikuwa nafikiria sana kuhusu hukumu ya City," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari jana Jumanne kuelekea mchezo wake dhidi ya Norwich City.

"Nilikuwa sijui sana kuhusu kesi yao, mimi nilikuwa naangalia zaidi matokeo ya timu ya na si vinginevyo.

"Tutapambana wenyewe kuhakikisha tunafuzu kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Chelsea inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England, kabla ya mchezo wa jana Jumanne.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOLSKJAER BADO ANA IMANI KUFUZU UEFA

Manchester United walikuwa na nafasi ya dhahabu kuimarisha matumaini yao ya kufuzu...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amebaki na matumaini kuhusu timu yake kuwa na nafasi ya kumaliza kwenye nne bora baada ya sare ya Jumatatu ya 2-2 dhidi ya Southampton kwenye Ligi Kuu ya England.

United ambayo ipo kwenye kiwango bora kwa sasa, ilikosa nafasi ya kupanda nafasi ya tatu kwenye msimamo, baada ya bao la kusawazisha la dakika ya 96 lililofungwa na Michael Obafemi aliyetokea benchi na kuipa sare hiyo Southampton pale kwenye dimba la Old Trafford.

Baada ya wapinzani wake, Chelsea na Leicester City zote kupoteza wikiendi, United walikuwa na nafasi ya dhahabu kuimarisha matumaini yao ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, ikiwa ni mechi ya 35 kwenye ligi hiyo.

**Walianza kutanguliwa kufungwa kwa bao la Stuart Armstrong, United walionekana kuwa kwe nye nafasi nzuri ya kuz ipiku Leicester na Chelsea shukrani kwa mabao ya Marcus Rashford na An thony Martial.**

Lakini United walishindwa kulinda ushindi wao dhidi ya Southampton, ambao walitumia dakika sita za nyongeza baada ya kutolewa kwa Brandon Williams aliyeumia kichwa na kuwaacha 'Mashetani Wekundu' hao na wachezaji 10 uwanjani.

Hata hivyo, Solskjaer alitetea timu yake baada ya kufikisha pointi sawa na Leicester wanaoshika nafasi ya nne, wakizidiwa moja na Chelsea waliopo nafasi ya tatu.

"Kwa hakika hapana," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari wakati alipoulizwa kuwa United kumefifisha matumaini kwa kushinda kuipiku Chelsea.

"Sidhani kama kuna mchezaji wetu yeyote anafikiria hilo, 'Oh kile Chelsea walichokifanya wikendi. Hapana."

"Ni namna mchezo ulivyokwenda na tulicheza na timu ile ile na tuna mechi 38 kwa msimu wote. Unastahili kuwa kwenye nafasi iliyopo mwishoni."

## ZISIKUPITE

### GUARDIOLA, CITY KUTETA

MANCHESTER City itampa ofa Pep Guardiola ili kuongeza mkataba wake baada ya kufutiwa adhabu ya kufungiwa kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mirror)***

### MBAPPE AVUTIWA PUMZI

REAL Madrid wanajiamini mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 21, atafikia makubaliano nao ya usajili kutoka Paris St-Germain miaka michache ijayo. ***(Marca)***

### LIVERPOOL KUMUUZA LOVREN

KLABU ya Liverpool inaangalia uwezekano wa kumuuza mlinzi wa kimataifa wa Croatia, Dejan Lovren mwenye umri wa miaka 31, licha ya kutaka kuongeza mkataba wake. ***(Goal)***

### KOULIBALY AWINDWA CITY

MLINZI wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 29, anaweza kuwa kwenye mipango ya kocha wa Manchester City, Pep Guardiola ili kuimarisha beki yake msimu ujao. ***(Telegraph)***

### NEYMAR AKATALIWA BARCA

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu amekataa uwezekano wa nyota wa Paris St-Germain, Neymar mwenye umri wa miaka 28 raia wa Brazil, kurudi Nou Camp, lakini amesema klabu inafikiria usajili wa straika wa Inter Milan na Argentina, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 22. ***(TV3 via Mundo Deportivo)***

### MESSI HADI MWAKANI

JOSEP Maria Bartomeu amesema "ana uhakika" mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, atabaki Nou Camp hadi mwakani. ***(TV3 via Evening Standard)***

### CITY KUTINGISHA SOKONI

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan na Argentina, Lautaro Martinez, 22, mlinzi wa Bayern Munich na Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, na straika wa Valencia, Ferran Torres mwenye umri wa miaka 20, wote wanahusishwa na Manchester City. ***(Mail)***

### NICE NA OFA KWA LOPES

KLABU ya Nice imetuma ofa kwa kiungo wa Hispania, Rony Lopes mwenye umri wa miaka 24 anayekipiga kule Sevilla. ***(RMC Sport)***

### AKE NJE MSIMU MZIMA

MLINZI wa Bournemouth, Nathan Ake raia wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 25, inawezekana asicheze tena msimu huu baada ya kuumia kwenye mchezo dhidi ya Leicester. ***(Bournemouth Echo)***

### NYOTA NORWICH SOKONI

MKURUGENZI wa michezo wa Norwich City, Stuart Webber amesema ofa ya kuwanunua wachezaji wao vijana kutoka klabuni hapo itaanzia pauni milioni 20 kwa kila mmoja. ***(Norwich Evening News)***

### CURTIS SASA AWINDWA

BRENTFORD inawania kumsajili winga wa Portsmouth, Ronan Curtis, 24, raia wa Hispania ili kuchukua nafasi ya Said Benrahma mwenye miaka 24 raia Algeria anayeondoka hapo Bees. ***(The News, Portsmouth)***

## Selem View sasa yarejea kivingine

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Selem View imeonekana kurejea kivingine baada ya mapumziko ya mlipuko wa virusi vya corona kutokana na kupata ushindi katika mechi tatu mfululizo, huku ikiwa haijapoteza tangu Ligi Kuu Zanzibar iliporejea tena Julai Mosi.

Selem View ambayo ipo katika hatari ya kushuka daraja juzi ilifanikiwa kupata alama tatu baada ya kuifunga timu Kongwe katika medali ya soka Visiwani Zanzibar, timu ya Jamhuri kwa mabao 3-0 kwenye mchezo uliopigwa katika dimba la Gombani.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mustafa Hassan alisema malengo yake makubwa ni kuinusuru timu hiyo isishuke daraja licha ya kukabiliwa na mechi ngumu za mwisho ambazo anamalizia michezo yake na timu za Kisiwa cha Unguja.

"Wakati tunaanza ligi tulikuwa tunapata matokeo mabaya, mechi nyingi tulipoteza kwa kufungwa, tulizotoa sare zilikuwa kidogo sana ikilinganishwa na zile tulizopoteza, lakini hivi sasa tumeanza vizuri kwa nafasi tuliyopo tunahitaji ushindi, hata tukipata sare inatusaidia japo si malengo yetu," alisema.

Selem View itashuka tena dimbani kesho kupepetana na timu ya KMKM katika Uwanja wa Mau A Kisiwani Unguja, mchezo huo unatarajiwa kuwa mgumu kutokana na wapinzani wao hao kuwa katika mbio za ubingwa.

## Ndanda yataka za Prisons, Mbeya City

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Ndanda FC, Abdul Mingange amesema anaimani ya timu yake kubaki Ligi Kuu kwa kuwa tayari ameweka mipango yake kuhakikisha anapata pointi 12 katika mechi nne zilizobaki za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mingange alisema anahitaji kupata alama tatu muhimu katika mechi zao mbili za nyumbani ikiwamo leo dhidi ya Tanzania Prisons na kisha Mbeya City utakaochezwa Julai 18, mwaka huu.

Alisema kikosi chake kipo vizuri pamoja na wachezaji kuwa na morali ya kupambana kutafuta pointi muhimu ili kuendelea kujiweka katika nafasi nzuri.

"Tukifanikiwa kupata alama sita za nyumbani, mipango itageukia kwenda kutafuta pointi katika mechi mbili za ugenini dhidi ya Alliance na Mbao FC.

"Tupo nafasi ya 17 si sehemu nzuri maana waliopo chini wakishinda wanatushusha, nimeongea na wachezaji wangu kwamba sasa hatutaki kupoteza kitu, katika michezo hiyo, ikiwezekana kupata pointi 12," alisema Mingange.

Alisema ana imani na wachezaji wake na kwamba wamemhakikishia kupambana hadi mwisho kuona timu yao hiyo inacheza Ligi Kuu msimu ujao.

# KIGOGO MICHEZO AJITOSA UBUNGE WA KINONDONI

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga na mdau mkubwa wa soka nchini, Abbas Tarimba, amejitosa kwenye mbio za ubunge baada ya jana kuchukua na kurejesha fomu ya kuomba ridhaa ya kuteuliwa na CCM kugombea Jimbo la Kinondoni.

**Milango ya kuomba kuteuliwa kugombea ubunge kwa tiketi ya CCM kuelekea uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba mwaka huu, ilifunguliwa rasmi jana na Tarimba akawa miongoni mwa waliojitokeza kuomba ridhaa hiyo kwa chama chake.**

Nipashe ambalo jana lilitanda katika ofisi mbalimbali za chama hicho nchini ili kujua watiania wake, jana lilimshuhudia Tarimba akifika Makao Makuu ya CCM Mkwajuni, Kinondoni saa 2:00 asubuhi akiwa peke yake na kuingia ofisini kuchukua fomu hiyo kabla ya baadaye majira ya saa 3:00 kuirejesha.

Mara baada ya kurudisha fomu hiyo, Tarimba alisema kuwa anaamini ni muda muafaka kwake kuomba ridhaa ya chama chake kumteua kuwatumikia wakazi wa Kiononddoni baada ya kujitathmini kabla ya kuchukua maamuzi ya kuchukua fomu ya kugombea.

Tarimba, ambaye ni Mkurugenzi Uwekezaji wa SportPesa Tanzania, alisema amepanga kuwatumikia vizuri Wanakinondoni kwa kuhakikisha wanapiga hatua ya kimaendeleo endapo atapata ridhaa ya chama chake na baadaye kushinda katika uchaguzi huo.

Aliongeza kuwa anafahamu changamoto zote za wilaya hiyo kutokana na kuwahi kuwa Diwani wa Kata ya Hannanasifu, Kinondoni kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia 2005 hadi 2015.

"Nina uwezo wa kikazi na dhamira ya kuwatumikia Wanakinondoni, kwani nafahamu changamoto nyingi zilizokuwapo kwenye wilaya hii, hivyo sina hofu kwani nina sifa zote za mimi kugomea hapa.

"Mimi hapa Kinondoni siyo mgeni, nipo hapa ninaishi kwa muda mrefu, hivyo ninajua kitu gani ambacho wanakitaka wakazi wa wilaya hii, kikubwa niwaahidi mengi makubwa," alisema Tarimba.




Mwenyekiti wa zamani wa Klabu ya Yanga, ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi Uwekezaji wa SportPesa Tanzania, Abbas Tarimba, akizungumza na vyombo vya habari, jana, baada ya kurejesha fomu ya kuomba ridhaa ya kuteuliwa na CCM kugombea ubunge wa Jimbo la Kinondoni jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Ambani aing'ata Yanga sikio kuwika*

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA hatari wa zamani wa Yanga, Boniface Ambani ameonyesha kusikitishwa na timu yake hiyo ya zamani kufungwa mabao 4-1 dhidi ya watani zao wa jadi Simba na kuwataka viongozi wa klabu hiyo kusajili wachezaji wenye uwezo mkubwa wanaoendana na hadhi ya klabu.

Akizungumza kutoka nchini Kenya jana, Ambani ambaye ni mfungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2008/09, akipachika jumla ya mabao 18 akiwa na Yanga, alisema kwa sasa anavyoitazama Yanga ina wachezaji wengi ambao hawana hadhi ya kuichezea klabu kubwa kama hiyo.

"Niliwaona wakicheza na Kariobangi Sharks mwaka jana kabla ya msimu huu haujaanza, nilishangaa na nikatoa maoni yangu kwenye mtandao wangu wa kijamii kuhusu mapungufu makubwa ya kikosi, lakini nilikashifiwa sana na baadhi ya watu," alisema Ambani ambaye ni raia wa Kenya.

Mchezaji huyo ambaye amejinasibu pia kuwa pamoja na shughuli zake zingine amebaki kuwa shabiki mkubwa wa Yanga, alisema amesikitishwa mno timu hiyo kufungwa na Simba na kusema kuwa inafaa sasa kukifanyia mabadiliko makubwa kikosi hicho.

"Ikiwezekana wasisajili kabisa wachezaji 30, wasajili 25 tu, halafu ile gharama ya kusajili wachezaji watano, waiongezee kwa wachezaji hawa hawa 25 ili wapate nyota wenye gharama kubwa na wa viwango vya juu," alisema.

Ambani pia alikumbushia juu ya yeye kutoa tahadhari ya kutomsajili straika kutoka Ivory Coast, Gnamien Yikpe kutoka Gor Mahia ya Kenya, lakini alidharauliwa.

"Kila kitu nilichokuwa nikitolea ushauri au tahadhari, basi nilikuwa naandikiwa maneno makali na kukashifiwa kwenye mtandao wangu wa kijamii, maana hata hili suala la Yikpe, mimi nilitoa tahadhari ya kutomsajili, kwa sababu mimi namfahamu vizuri alikuwa hapa nchini Kenya akiichezea Gor Mahia, wananidharau na leo hii nadhani wameyaona," alisema straika huyo wa zamani wa klabu hiyo.

Michezo

Jumatano Julai 15, 2020

Nipashe



Solskjaer bado ana imani kufuzu Uefa

UKURASA 22

MSITU MNENE...



Mshambuliaji wa Southampton, Michael Obafemi (anayevutwa jezi) akiifungia timu yake bao la usiku [dk. 87] la kusawazisha huku akizingirwa na msitu wa wachezaji wa Manchester United, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa katika Uwanja wa Old Trafford juzi na timu hizo kutoka sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YATAJA WAKUSAJILIWA

## Wamo wa kimataifa wawili, straika na beki, huku pia ikimulika wengine kutoka...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuwaadhibu watani zao, Yanga kwa kipigo cha mbwa mwizi kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini maarufu FA Cup, mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba wametaja idara wanazotarajia kuziboresha katika kikosi chao kuelekea msimu ujao.

**Mwishoni mwa wiki Simba ilipata ushindi wa mabao 4-1 kwenye mechi hiyo ya nusu fainali dhidi ya Yanga iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, hivyo sasa itakutana na Namungo FC iliyoitoa Sahare All-Stars kwa bao 1-0.**

Mechi hiyo ya fainali ambayo inatarajiwa kuwa ngumu kutokana na ubora wa timu hizo mbili, itapigwa katika Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga mkoani Rukwa Agosti 2, mwaka huu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana kuhusu mpango wa kukiboresha kikosi chao, Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, alisema wanatarajia kuongeza wachezaji wasiozidi wanne katika dirisha la usajili lijalo ili kukiimarisha kikosi chao kuelekea michuano ya kimataifa, Ligi Kuu na michuano mingine msimu ujao.

Alisema lengo ni kutoharibu uelewano wa wachezaji uwanjani ambao tayari kocha ameutengeneza, hivyo wanachotazama ni kuongeza nguvu kidogo katika idara ya ushambuliaji na safu ya ulinzi.

"Hatuwezi kubadili timu nzima kama Yanga, matarajio yetu ni kusajili mabeki wawili ama watatu na washambuliaji wawili tu ili kuongeza nguvu," Manara alisema.

"Tutasajili mshambuliaji mmoja wa kimataifa na mmoja wa ndani na kwa upande wa beki ikiwezekana mmoja wa kimataifa na mwingine wa ndani, hatutaki kuwa kama Yanga ambayo msimu ujao unaweza kushuhudia ikisajili wachezaji 15 wapya [aliwananga watani zao]."

Simba ambayo tayari imetwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu, hiyo ikiwa ni kwa mara ya tatu mfululizo, itaiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Namungo FC ikiwa na tiketi ya kupeperusha bendera ya Tanzania katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika. Kwa upande wake Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amewapongeza wachezaji wake kwa kutoa dozi kwa Yanga juzi, huku akiwataka sasa kuelekeza akili zao kwenye mechi zilizosalia Ligi Kuu ili kumaliza msimu vizuri.

"Tulicheza vizuri na wachezaji walitimiza majukumu yao uwanjani na ndicho kimesababisha kupata ushindi mnono wa mabao 4-1 na kuleta furaha kwa Wanasimba wote," alisema.

Hata hivyo, raia huyo wa Ubelgiji alikiri kuwa Yanga ilikuwa bora zaidi katika dakika 15 za mwanzo ambapo walikuwa na kasi na kufanya mashambulizi ya haraka na baada ya kupata bao lao, lakini Simba ilikuwa bora katika muda wote uliobaki.

"Nimefurahishwa na jinsi ambavyo wachezaji wangu walivyocheza walijituma na walitimiza wajibu wao uwanjani kingine ni ushindi mnono tuliopata katika mchezo wa 'dabi' si jambo dogo hili, nawapongeza sana wachezaji wangu," alisema Sven ambaye kesho atakiongoza kikosi chake kuivaa Mbao FC katika mechi ya Ligi Kuu itakayopigwa Uwanja wa Taifa.

# Siri Yanga, Azam kuitaka nafasi ya pili

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Klabu ya Yanga na Azam zikipigana vikumbo kuwania kumaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu msimu huu, Nipashe limebaini siri kubwa inazozifanya klabu hizo kutoana jasho kuisaka nafasi hiyo.

Tayari Simba imetwaa ubingwa wa ligi hiyo ambayo imebakiza mechi nne kabla ya kumalizika msimu huu, hivyo kujihakikishia nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye Kombe la Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika, timu yenye tiketi hiyo nchini, ni Namungo FC ambayo imetinga fainali ya Kombe la FA na sasa itakutana na Simba Agosti 2, mwaka huu katika Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga mkoani Rukwa, hivyo hata kama Wekundu wa Msimbazi wakishinda uwakilishi huo utabaki kwa Namungo kwa kuwa yenyewe itaiwakilisha nchi Ligi ya Mabingwa.

Hata hivyo, wakati akizungumza na mwandishi wetu jana kuelekea mchezo wao wa leo utakaopigwa katika Uwanja wa CCM Gairo mkoani Morogoro dhidi ya Mtibwa Sugar, Kocha Mkuu wa Azam FC, Mromania Aristica Cioaba, alisema malengo yake ni kushika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu ili kama Tanzania itapata tena nafasi nne za kushiriki mashindano ya kimataifa bahati hiyo iwaangukie.

Alisema mipango yao imevurugika kutokana na kutolewa kwenye michuano ya FA Cup, lakini watahakikisha sasa wanamaliza wa pili ili kuvizia nafasi hiyo endapo itajitokeza tena kama msimu uliopita.

Azam FC ipo nafasi ya pili ikiwa na alama 65 baada ya mechi 34, ikiwa ni pointi moja mbele ya Yanga ambayo nayo itashuka katika Uwanja wa Taifa leo kuikaribisha Singida United inayoburuza mkia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >